ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.

12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/\Jimbo la Jang'ombe.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.

23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais

37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Nane – Tarehe 20 Disemba, 2013

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Hati Mezani Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Hati Miliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Hati Mezani Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Karafuu Nam. 11 ya mwaka 1985 na Kuweka Sheria Mpya ya Maendeleo ya Karafuu na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha Hati Mezani Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Nyumba Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 7

Doria Mji Mkongwe

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Hivi karibuni kumejitokeza wimbi la matukio ya kihalifu katika sehemu mbali mbali nchini yakiwemo maeneo ya Mji Mkongwe ambapo kumewahi kutokezea matukio ya uhalifu kwa wananachi na wageni kama vile kumwagiwa tindi kali na kadhalika.

(a) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina mpango gani wa kuweka doria saa 24 katika mitaa mbali mbali ya Mji Mkongwe.

(b) Kwa kuwa taa ni muhimu katika mambo ya usalama, lini serikali itaondoa tatizo la ukosefu wa taa katika mitaa ya Mji Mkongwe kwa usalama wa wageni na wananchi wake.

(c) Je, serikali imechukua hatua gani za kuwajengea uwezo Polisi Jamii katika kukabiliana na vitendo vya uhalifu katika Mji Mkongwe ambao ni kivutio kikubwa katika sekta ya Utalii Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 7 lenye vifungu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, serikali kupitia Jeshi la Polisi imekuwa ikifanya doria saa 24 katika maeneo ya Mji Mkongwe. Doria hizo zina lengo la kuzuia au kupunguza uwezekano wa kutokea uhalifu. Lakini wahalifu wamekuwa wakitumia maficho na mbinu za kushtukiza, ambazo askari wetu wa Doria inakuwa ni vigumu kuzijua kwa haraka.

Kwa hivyo, natoa wito kwa wananchi wote kushirikiana na Jeshi la Polisi pamoja na Polisi Jamii katika kutoa taarifa yote yote ile inayotia mashaka ya kutokea uhalifu au kumtilia mashaka mhalifu, hasa watu ambao ni wageni katika maeneo yetu tunayoishi.

b) Serikali inafahamu umuhimu wa kuwekwa taa katika maeneo yote ya mji wetu kwa lengo la kuweka usalama kwa wageni na wananchi wetu kwa jumla. Serikali imeanza kazi hiyo kwa kuchukua hatua za kuweka taa kwa maeneo ya barabarani na Wajumbe wa Baraza lako ni mashahidi wa hilo. Aidha serikali kupitia Baraza la Manispaa limepokea ushauri wa Mhe. Mjumbe na kuufanyiakazi kadri inavyowezekana kwa usalama wa wageni na wananchi wetu. *(Makofi)*

c) Mhe. Spika, serikali kwa mashirikiano na Makao Makuu ya Polisi Zanzibar imewajengea uwezo Polisi Jamii katika kukabiliana na vitendo vya uhalifu katika Mji Mkongwe, ambao ni kivutio kikubwa katika Sekta ya Utalii, kwa kuwapatia mafunzo ya kuwatambua na kuwafuatilia wahalifu, elimu ya ukakamavu na ukamataji salama pamoja na elimu ya Haki za Binadamu.

Kwa hivyo, nalipongeza sana Jeshi la Polisi pamoja na Polisi Jamii kwa hatua ya kufanyakazi nzuri katika maeneo yetu na kupunguza uhalifu na vitendo viovu katika miji yetu. Mhe. Spika, napenda nichukue fursa hii kuwashukuru wale wananchi wote wanaoshirikiana na Jeshi la Polisi katika kupambana na uhalifu nchini.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri na ushauri amesema kwamba ameupokea.

a) Kwa hiyo, pamoja na ahadi za kuufanyiakazi ushauri huo wa kufunga taa wananchi wanataka kufahamu, ni lini wataondoka kwenye giza katika Mji Mkongwe wa Zanzibar wakati ndio kivutio namba moja cha utalii wetu wa Zanzibar.

b) Kwa nini Polisi Jamii wamekuwa wakilalamikiwa kuchukua madaraka mikononi mwao kinyume na misingi ya Haki za Kibinadamu kama wamepatiwa mafunzo ya utekelezaji wa shughuli zao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika,

a) Kutokana na nilivyosema katika jawabu langu la msingi kwamba serikali imeanza hatua ya kuweka taa barabarani na ina mpango mkubwa wa kuweka taa hizo katika Mji Mkongwe na maeneo mengine ya nchi yetu. Msingi wake inaelewa umuhimu wa taa hasa katika Mji wetu Mkongwe.

   Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Mjumbe, avute subira wakati mradi huo unaendelea, kwa sababu zipo fedha za *World Bank* zimetolewa kama dola milioni 38 kwa ajili ya kuendeleza masuala mbali mbali ya Manispaa ikiwemo suala zima la kuweka taa katika Mji wetu huu wa Zanzibar. Hata hivyo, suala la Mji Mkongwe litafikiriwa zaidi na kwa kuwa Mhe. Waziri mhusika yupo hapa kama atakuwa na maelezo ya ziada atalielezea.

b) Aidha kuhusu Polisi Jamii kuchukua mamlaka mikononi mwao. Kwa kweli hivyo sivyo walivyofundishwa Polisi Jamii Mhe. Spika, isipokuwa walivyofundishwa ni kama nilivyosema hapa kwamba wamefundishwa suala la ukamataji salama. Ukamataji salama maana yake hutakiwi kumpiga au kumdhalilisha raia mwengine, lakini unatakiwa umkamate kwa taratibu zilizopo na ikiwa huyo mhalifu

ataleta matatizo basi pia unatakiwa umuachie na uendelee kuripoti polisi.

Kwa hivyo, hakuna haki ya mtu yeyote yule hasa kwa kumuonea mtuhumiwa kwa kumpiga au kufanyia jambo jengine lolote mpaka pale utaratibu wa sheria utakapochukua mkondo wake, na ni mahakama pekee ndio yenye uwezo wa kutoa hukumu nani apewe hukumu gani. Kutokana na hali hiyo, si vizuri kuchukua sheria mikononi mwetu, kwani kuchukua sheria mikononi ni kosa kwa mujibu wa sheria.

Nam. 57

Usimamizi wa Fedha za Mfuko wa Jimbo

Mhe. Salma Mussa Bilal - Aliuliza:-

Kwa kuwa Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imekuwa ikitoa fedha za Mfuko wa Jimbo kwa Wawakilishi wote wa Majimbo.

(a) Je, wizara yako inahakikishaje kwamba fedha hizo zinatumika ipasavyo.

(b) Je, kuna utaratibu gani uliopangwa wa kufuatilia usahihi wa matumizi ya fedha hizo.

(c) Kwa kuwa Wajumbe wa Viti Maalum vya Wanawake nao wanakabiliwa na majukumu makubwa ya kuwahudumia wanawake katika Mikoa yao ambayo yanabeba majimbo yote yaliyomo katika Mikoa hiyo. Je, wizara yako haioni kama kuna haja na wao kupatiwa mfuko huo, hasa kwa kuzingatia wao wana eneo kubwa (Mkoa) zaidi kuliko Wawakilishi wa Majimbo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 57 lenye vifungu (a), (b) na (c) naomba nitoe maelezo ya awali.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imekuwa ikitoa fedha kwa ajili ya maendeleo ya majimbo yetu yote ya Unguja na Pemba. Lengo la fedha hizi ni kwa ajili ya kutekeleza miradi mbali mbali ya maendeleo kwa wananchi katika majimbo yao. *(Makofi)*

Fedha hizi zinazotolewa kwa ajili ya maendeleo ya jimbo ni fedha za serikali na hazina budi zifuate sheria na kanuni na taratibu za matumizi ya serikali.

Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Nam. 4 ya mwaka 2012, ambayo tumeipitisha sote kwa pamoja ndani ya Baraza hili, pamoja na mambo mengine imeweka utaratibu wa kuwashirikisha wananchi katika kuibua, kutekeleza pamoja na kusimamia miradi inayotekelezwa ndani ya majimbo yetu. Aidha sheria hii imeeleza utaratibu wa kufanya matumizi kama ilivyokawaida ya fedha za serikali.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 57 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambayo imepewa jukumu la kuratibu fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, inafuatilia miradi iliyotekelezwa ndani ya majimbo na shughuli hii tayari imeshafanyika. Maofisa wameshaanza kazi ya kuyapitia majimbo ya Unguja na kazi hii pia itafanywa kwa majimbo ya Pemba. Aidha Wizara ya Fedha kupitia Mkaguzi wa Hesabu za Serikali nae atapita, ili kukagua miradi iliyotekelezwa pamoja na kulinganisha thamani ya fedha iliyotumika.

b) Mhe. Spika, kama kawaida ya fedha za serikali zinapotumika ni lazima ziwe na marejesho, ili kuthibitisha uhalali kilichonunuliwa au kilichofanyika. Kwa hivyo, matumizi ya fedha hizi pia yanahitaji marejesho ya kuthibitisha uhalali wa kilichonunuliwa. Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais inapitia marejesho yote yaliyowasilishwa kwa ajili ya kutoa fedha nyengine za maendeleo ya jimbo, ili iweze kutekelezwa miradi mingine.

c) Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo imepitishwa na Wajumbe wa Baraza lako mwaka 2012 na bado inaendelea kutathminiwa utekelezaji wake, iwapo sheria kuna haja ya kuifanyia mabadiliko kwa lengo la kuiboresha zaidi, basi taratibu zitafuatwa ili iweze kuleta manufaa zaidi. Kwa sasa kutokana na uwezo mdogo wa fedha serikalini, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wakubaliane na utaratibu uliopo, ambao utanufaisha shughuli za majimbo tu na bado kwa Viti Maalum Wanawake.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashkuru kupata nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, wakati tulipokuwa tukipitisha matumizi katika Mfuko huu wa Jimbo tulikuwa na mvutano mkubwa kuhusu

kutumika kwa kujenga kama vile misikiti na vyuo, lakini mwisho wake tukakubaliwa.

Sasa kwa bahati mbaya katika semina waliofanyiwa Makatibu wa Mfuko huu wa Majimbo walielezwa huko kwenye semina kuwa kutoa fedha kwa ajili ya misikiti, vyuo na vikundi vya watu binafsi hairuhusiki isipokuwa ni kwa miradi mikubwa tu ambayo ni ya kudumu.

Je, Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri, hivi kuna mamlaka yoyote ya kutengua yale maamuzi ambayo sisi hapa tumeyapitisha bila ya kurudi hapa. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, sheria inayopitisha na Baraza hili tukufu Mhe. Spika, hakuna mtu mwengine anayeweza kuitengua isipokuwa kuja tena kwenye Baraza hili na kufanyiwa marekebisho. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kuwa Tume ya Mabadiliko ya Katiba imependekeza Viti Maalum vifutwe wajumbe kupitia nafasi hizo, serikali imechukua hatua gani kuangalia utaratibu huo. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, nafikiri hili ulitafutie utaratibu wa kuuliza swali la msingi. *(Kicheko/Makofi)*

Nam. 51

Ahadi ya Mhe. Waziri Kukutana na Wafanyabiashara Wadogo

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Wafanyabiashara wadogo wadogo katika viwanja vya Forodhani walipata faraja kubwa baada ya aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais mwenye dhamana ya Vikosi vya SMZ na Manispaa alipoahidi kukaa pamoja kuzungumzia tatizo la ada kubwa wanayotozwa wafanyabiashara katika eneo hilo.

(a) Kwa nini ahadi hiyo haijatekelezwa wakati wafanyabiashara, wanaendelea na kilio chao cha kutozwa ada, ambayo haisaidii kumuinua mfanyabiashara mdogo.

(b) Je, katika mazingira kama hayo serikali imesaidia vipi utekelezaji wa Mpango wake wa Kukuza Uchumi na kupunguza Umasikini kwa wananchi wake (*MKUZA*).

(c) Kwa kuwa suala hili ni zito kutokana na kuwa linagusa mambo ya msingi ya mahitaji ya wananchi wetu wizara itatekeleza vipi ahadi ya serikali ya kukutana na wafanyabishara, ili kuwaondolea unyonge huo.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ- Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 51 lenye kifungu (a), (b) na (c), lakini kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Bustani ya Forodhani ni bustani iliyotengenezwa kwa gharama kubwa na ilijengwa na Wafadhili. Kwa dhana ya kuona bustani hiyo haipotezi haiba yake na ni moja ya maeneo tuliyokubaliana na Mfadhili huyo namna au jinsi bustani hiyo itakavyotunzwa muda wote.

Ili kuweka usimamizi bora na wa pamoja, Bodi Maalum iliundwa kusimamia mwenendo mzima wa bustani na uendeshaji wake. Miongoni mwa Wajumbe wa Bodi ya Bustani ya Forodhani ni Mamlaka ya Mji Mkongwe, Mwakilishi wa Agakhan na Baraza la Manispaa. Uendeshaji wa Bustani hiyo unahitaji fedha nyingi ikiwemo kulipia huduma ya umeme, maji, matunzo ya bustani yenyewe, ulinzi na shughuli nzima ya usafi kwa kila siku ambazo kwa wastani zinatumika shilingi 3,308,000/= kwa mwezi (bila ya gharama za maji) na mapato ni wastani wa shlingi 3,830,800/=.

Baada ya maelezo hayo naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

(a) Tarehe 18/7/2013 kilifanyika kikao kati ya Bodi ya Forodhani kwa upande mmoja na wafanyabiashara wa Forodhani kwa upande wa pili, pamoja na mambo mengine yaliyozungumzwa, mada ya kupunguziwa malipo ilijadiliwa. Kutokana na gharama kubwa za uendeshaji wa Bustani hiyo kuwa kubwa haitakuwa busara kuvipunguza viwango hivyo na Bodi inafikiria kuviongeza kwani ni vidogo.

(b) Miongoni mwa suala kubwa lililojitokeza katika *MKUZA* ni suala zima la ajira, katika hili serikali imeweza kujenga mazingira mazuri ya vijana na wananchi kwa ujumla kujiajiri wenyewe baada ya kuimarisha mazingira ya Bustani ya Forodhani, ambapo kwa sasa eneo hilo linaleta haiba nzuri na kuwa ni kivutio kikubwa cha watalii kiasi kwamba vijana wetu wanauza vyakula, walinzi na madereva wameweza kujiajiri na kujipatia kipato cha kuendeleza maisha yao

binafsi na pia kuchangia katika maendeleo ya nchi kiujumla na kupunguza umaskini.

(c) Kama nilivyosema katika jibu (a) serikali inakutana na wananchi wanaofanya biashara na tayari makubaliano yamefikiwa katika kikao cha Bodi ya Bustani siku ya tarehe 18/7/2012 ifahamike kwamba Bodi hiyo inafanyakazi kwa niaba ya serikali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana kwa vile hii ilikuwa ni ahadi ya Mhe. Waziri, kukaa na wafanyabiashara hao na Mhe.Spika, wafanyabiashara wenyewe wapo pale wamekuja kusikiliza kilio chao. Kwa kweli hoja ilikuwa ni shilingi 90,000/= ni sehemu au meza ndogo tu, umeme ni wao na kama kuna mvua ama jua hakuna mwavuli vyakula vikitoa au havikutoka na ahadi ilikuwa ni Mhe. Waziri, kukaa na wafanyabiashara na wala sio bodi wala mamlaka nyengine na *hansard* ninayo Mhe. Spika, na kwa ruhusa yako naomba kuinukuu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, hoja mbili zimeshasemwa kwa hivyo utajibiwa hoja moja kuhusu shilingi elfu 90,000/=.

Mhe. Waziri wa Nchi na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kuhusu lile punguzo, suala hili inabidi waache tukae, kwa sababu mimi sina mamlaka ijapokuwa ni waziri ndio, lakini kuna Baraza linakaa kwa ajili ya kuyazingatia na kuyafanyiakazi. Kwa hivyo, nasema ushauri wake tunauchukua wacha tukakae na wenzetu tuone tunaweza tukawafahamisha.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kikao kinaweza kuchukua muda, basi mimi aniambie tu kama kesho au kesho kutwa ama baada ya wiki (anipe muda) ili niweke kumbukumbu sawa. Kwa kweli najua kikao kinaweza kuchukua muda na ukaambiwa serikali iko mbioni uzoefu tumeuona katika Baraza hili.

Mhe. Waziri wa Nchi na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ushauri wa Mhe. Jaku Hashim Ayoub,tumeupokea na tuko tayari kukaa wiki moja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kwa hivyo, Mhe. Spika ahadi ya Mhe. Waziri, ipo pale pale kukaa na wafanyabiashara na wala sio Bodi. Kutokana na hali hiyo, nimuombe Mhe. Waziri, kwa heshima na taadhima ya hali ya juu kupitia kwako Mhe. Spika, wale jamaa kilio chao sio kwenda kutafuta muhogo. Kwa hiyo, ninaomba sana awasaidie kutoka shilingi 90,000/= angalau shilingi

70,000/=, kwa sababu ile meza inakodiwa shilingi 4,000/= kupeleka na kurejeshwa.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, swali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kilio kikubwa cha wafanyabiashara ni kupunguziwa ile kodi. Kwa kweli sijui anatoa kauli gani na wafanyabiashara wenyewe wapo pale wanasikia.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, swali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, swali pamoja na maelezo ya Mhe. Waziri, kwa kuwa ahadi ni deni aliyekuwa waziri dhamana katika Baraza hili wakati wa Bajeti lililopita, alisema atakutana na wafanyabiashara na sasa hakuna utekelezaji wake. Je, lini litatekelezwa suala hili. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, hivi sasa katika kuuliza swali hili amefayakazi ya kutekeleza wajibu wake katika kulitumikia taifa lake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza katika jibu mama ahadi ya waziri aliyoitoa Barazani nakubaliana naye kwamba iko pale pale. Lakini nchi hii inakwenda kwa mujibu wa taratibu na sheria na makubaliano yaliyowekwa wenye mamlaka ya uendeshaji wa Bustani ile ya Forodhani ni Bodi ya Bustani ya Forodhani, ambayo bodi hiyo vile vile inateuliwa na Waziri anayehusika na Masuala ya Mji Mkongwe na wala sio Tawala za Mikoa na Idara Maalum za *SMZ.*

Kwa hiyo, mimi nadhani kwanza hiyo bodi iliundwa tarehe 30 Julai, 2009 na kinachoonekana kwa mujibu wa utaratibu wa bodi hiyo, bodi hivi sasa imeshamaliza muda wake. Kutokana na hali hiyo, taasisi inayohusika itachukua hatua ya kuweza kuunda bodi hiyo upya, ili iweze kutekeleza majukumu yake vizuri.

Lakini ieleweke kwamba pale kuna taasisi mbili zinazosimamia shughuli za uendeshaji wa Bunstani wa Forodhani. Kwa mfano kuna hii bodi ambayo yenyewe ndio inayokusanya mapato na kuna Baraza la Manispaa, ambalo linaimarisha usafi na kusimamia Bustani ya Forodhani. Bodi inakusanya mapato na kuyatumia kuendesha gharama za uendeshaji kwa ajili ya kuwalipa wafanyakazi 16 waliowaajiri. Baraza la manispaa linaimarisha bustani na usafi, ambalo nalo pia linao wafanyakazi 16 pale. Fedha zinazokusanywa hakuna hata senti tano inayokwenda katika Baraza la Manispaa. Kwa maana hiyo, wafanyakazi wanaoshughulikia bustani, usafi pamoja na magari

yanayokuja kuchukua taka zinazotoka pale zinagharamiwa na Baraza la Manispaa. Kwa hivyo, hivi ni vitu viwili tofauti.

Mhe. Spika, naomba Mhe. Mjumbe afahamu kwamba wafanyabiashara na Bodi inayoendesha Bustani ya Forodhani wakifikia pahala wakikubaliana kwamba wapunguziane na hilo litakuwa ni suala jengine. Lakini Waziri au Baraza la Manispaa halina mamlaka katika suala hilo, isipokuwa yenye mamlaka ni Bodi.

Sasa pale aliposema kwamba bado ahadi inabakia pale pale, mimi kwa sababu nasimamia bustani pamoja na usafi, basi nitajipa kazi hiyo ya kwenda kukutana na wafanyabiashara tuzungumzie juu ya uendeshaji wa bustani pamoja na *parking* ya Forodhani, lakini sina mamlaka ya kupunguza viwango.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri, siku hiyo atakayokutana na wafanyabiashara wa Forodhani na mimi anialike.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, sijakufahamu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri, siku atakayokutana na wafanyabiashara wa Forodhani kama alivyosema kwamba ahadi ipo pale pale kwamba atakaa na wafanyabiashara, basi na mimi naomba anialike.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Wakati Mhe. Waziri, alipokuwa akijibu swali la msingi alisema kwamba michango inayotolewa na wafanyabiashara pale ni kwa ajili ya kuitunza bustani ili isipoteze haiba yake ya awali.

a) Pamoja na michango inayotolewa na wafanyabiashara na kwa ajili ya maegesho. Mhe. Waziri, atakubaliana na mimi kuwa bustani ile hivi sasa imeshapoteza haiba yake. *(Makofi)*

b) Nini kifanyike, ili bustani ile iweze kurejesha haiba yake ya awali na wakati ilipokuwa ikifunguliwa ilikuwa inavutia machoni mwa watu. Lakini inaonekana hivi sasa imeshapoteza ile haiba iliyokuwepo mwanzo. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, swali la kwanza naomba alirejee.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, rejea swali la (a).

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika.

a) Mhe Waziri, atakubaliana na mimi kwamba ile bustani pamoja na michango inayotolewa ambayo inalalamikiwa hivi sasa, bustani imeshapoteza haiba yake.

b) Nini kifanyike, ili bustani ile iweze kurejesha haiba yake ya awali na wakati ilipokuwa ikifunguliwa ilikuwa inavutia machoni mwa watu kwani inaonekana hivi sasa imeshapoteza ile haiba iliyokuwepo mwanzo, pamoja na hizo fedha ambazo zinazochangiwa. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, anasema Mhe. Mjumbe kwamba bustani imepoteza haiba yake. Kwa kweli ieleweke kwamba bustani ile ilipoimarishwa kwanza ilipandwa majani ya kigeni kutoka nje, majani ambayo hayaendani na hali halisi ya hewa ya nchi yetu. Majani yale wakati wa mvua kama hizi yanakuwa yanaonekana yanaimarika, tena ni majani ambayo hayahimili vishindo.

Kutokana na tabia zetu sisi wananchi ambao hatupendi kufuata utaratibu kikamilifu tunajikalia ovyo kwenye bustani, ama majani yale, na tunaacha yale maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya kukaa au kupita na badala yake tunavuruga ile bustani.

Kwa hiyo, ni kweli katika hali isiyo ya kawaida bustani ilipoteza haiba yake, lakini sababu ya msingi ni hio nilioieleza.Hata hivyo, nini kifanyike. Wizara yangu kwa kupitia Baraza la Manispaa, imeamua kubadilisha majani yaliyokuwa yamepandwa mwanzo na kupanda majani ambayo yanahimili hali ya hewa ya hapa kwetu Zanzibar.

Nini kifanyike ni kwamba wizara yangu itakaa pamoja na wahusika wengine, kwa maana ya ile Bodi inayohusika na bustani hii, tuone ni kwa jinsi gani tunaweza tukaiendeleza ile bustani. Hivi sasa Mhe. Spika, ile bustani ina kasoro nyingi, hata ile mifereji iliyowekwa kwa ajili ya kumwagilia maji, wananchi wamekuwa wakiikata. Hiyo inatokana na zile zile khulka za kutokubadilika.

Kwa hivyo, wizara yangu kwa kupitia Baraza la Manispaa kwa sababu ndio lenye jukumu la kuweza kutunza bustani, itafanya utaratibu wa kuweza

kuirejesha mifereji ile na itawasiliana na Mamlaka ya Maji ili kuona maji yanapatikana kwa muda wote ili tuweze kuirejesha haiba ya bustani ile.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa muda huu kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Waziri serikali kila siku inasema vijana wajiajiri. Mhe. Spika, vijana wamekubali kujiajiri wao wenyewe. Kutokana na jibu lako la swali mama ulisema kuwa bado Bodi inataka kuongeza kodi kwani ile iliyopo sasa hivi ni ndogo.

a) Je, Mhe. Waziri huoni ni kuwadhalilisha vijana kwa kuwaongezea kodi, baada ya hiyo iliyopo sasa hivi.

b) Mhe. Waziri, wizara yako haioni huruma kwa kuongeza kodi mara tatu zaidi kuwa ni kuwarudisha vijana katika *jobless* na kuwepo kuongezeka uwizi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwanza serikali kwa kupitia wizara yangu, hata siku moja haitofanya maamuzi ya kuwadhalilisha vijana wa Zanzibar, hasa wale wanaoamua kujitafutia riziki kwa kujiajiri wenyewe. Kilichopo hapa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, ni utaratibu na makubaliano ya uendeshaji wa bustani ya Forodhani, kwamba bustani ile inatakiwa ijiendeshe kwa gharama zinazotokana na ada inayotozwa pale.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo kuwa Baraza la Manispaa halichukui *single pan* kwa ajili ya kuendesha shughuli zake. Bado Baraza la Manispaa linatoa fedha kwa kuwalipa wafanyakazi 16 wanaosafisha na wanaoitunza bustani. Katika fedha ambazo zinazotolewa kama nilivyosema mwanzo ni milioni 3,830,000,000, ukitoa milioni 3,308,000,000, kinachobakia ni shilingi 522,000. Hizo haziendi kabisa kwenye mfuko wa Baraza la Manispaa, zinabakia kwenye Bodi kwa ajili ya kuangalia ni tatizo lipi kubwa ambalo zinaweza kutumika hizi, zinazobakia kuiendeleza na kuifanya ile bustani ibaki na haiba yake.

Mhe. Spika, hivi sasa kuna tabia ya wenye vyombo kufunga boti zake kwenye ukuta wa bustani, jambo ambalo haliruhusiwi, wanaharibu bustani ile. Hizi shilingi 500,000 zinazobakia iwapo uharibifu kama huu utakuwa unafanyika basi zitatumika kwa ajili ya kuiendeleza. Sasa sijui serikali ingefanya wema gani kwa vijana wake, badala ya zile fedha zinazozalishwa, ikatoa na pesa zake kuwalipa mshahara wafanyakazi ambao wanaitunza ile bustani. Kwa hivyo, serikali inawajali sana vijana wake. Ahsante sana Mhe. Spika.

Nam. 62

Ongezeko la Vyombo vya Moto na Ufinyu wa Barabara

Mhe. Fatma Mbarouk Said – Aliuliza:-

Kwa kuwa Zanzibar imo katika nchi zinazoendelea kwa kila sekta na mji wetu kuwa na ongezeko la vyombo vya moto.

(a) Ni lini Serikali itazingatia suala la "*road reserve*".

(b) Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kujenga barabara za juu (Flying Over).

(c) Ni lini Serikali itaweka taa za kuongozea magari katika makutano ya barabara mbali mbali baada ya kuharibika taa zilizopo miaka mingi iliyopita.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 62 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, wizara yangu tayari imeshawasilisha Barazani Marekebisho ya Sheria ya Barabara (*Road Decree Cap. 134*) ya mwaka 1925. Katika marekebisho hayo moja kati ya mambo ambayo yameelezwa kwa uwazi ni mipaka ya maeneo ya hifadhi ya barabara.

Aidha, serikali tokea mwaka 1927 imekuwa ikizingatia eneo la hifadhi ya barabara. Mabadiliko tuliyoyafanya ni namna ya kuongeza maeneo ya hifadhi hiyo ya barabara.

(a) Mhe. Spika, nakubaliana na wazo la Mhe. Mjumbe na wizara yangu italifanyia kazi. Tutalifanyia kazi hatua kwa hatua kuendana na mabadiliko na maendeleo ya nchi yetu.

(b) Mhe. Spika, kwenye mwaka wa fedha 2013/2014 kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imepanga kuweka taa zinazotumia nguvu za jua (*Solar Power*) za kuongozea magari pamoja na *CCTV* camera kwenye makutano ya

barabara ya Malindi, Mkunazini na kwa Mchina mwanzo. Aidha wizara itaendelea kuweka taa kama hizo sehemu mbali mbali ya makutano ya barabara kwa Unguja na Pemba kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara kadri hali ya kifedha itakayvoruhusu.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi tena ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa taa za kuongozea magari ni muhimu katika makutano ya barabara na kwa sababu mambo haya ni ya kiufundi zaidi.

Je, serikali ina mpango gani kabla ya wataalamu kuondoka ikawapa mafunzo ya kiufundi mafundi wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, azma yetu ni kuweka taa katika maeneo yetu ambayo tumeyataja. Sisi kama serikali ni lazima twende hatua kwa hatua. Hatua yetu ya awali ni kuhakikisha kwamba wataalamu hawa wanakuja na wataungana na wataalamu wetu katika kutengeneza.

Suala la mafunzo ni wajibu wetu. Tutawachukua wataalamu wetu waende wakajifunze namna ya uendeshaji na uimarishaji kwa kushirikiana na wenzetu wa manispaa, kwa sababu wao ndio wenye dhamana ya kuzitunza na kuendeleza mradi huu wa taa za usalama wa barabarani.

Mhe. Asha Abdu Haji: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa tuna sherehekea sherehe za kutimia miaka 50 ya Mapinduzi, na kwa kuwa taa za barabarani kuanzia Amani na kuelekea Mjini hazifanyi kazi, je, serikali haioni aibu kwa suala hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, mimi naamini kwamba suala lake Mhe. Mwakilishi moja kwa moja ni jukumu la wenzetu wa manispaa, suala hili la uwekaji wa taa hizi za barabarani ili kuweza kutoa mwanga. Lakini kwa sababu ameelekeza hoja yake kwa upande wa serikali, basi tunaamini kwamba sisi tuna wajibu wa kuwakumbusha wenzetu wa Manispaa, ili kutimiza wajibu wao huo kwa kuweka taa hizo, ili barabara zetu ziweze kuonekana na watu waone jitihada za uwekaji wa lami safi na salama na barabara bila mashimo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mara nyingi huwa napenda kuuliza swali dogo sana la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri katika jibu lako zuri ulilojibu, ulisema kwamba sasa hivi wizara yako ina mpango wa kuleta taa za kisasa na kamera na kila kitu.

Je, Mhe. Naibu Waziri hivi sasa barabara zetu bado zina *modality* za kizamani na ni mbovu. Huoni iko haja kabla ya kwenda huko kununua taa, pesa hizo ukazitengenezea barabara katika maeneo ambayo umeyakusudia.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, miradi ya barabara ni miradi endelevu, barabara inajengwa, barabara inatumika na bila shaka ikitumika itaathirika. Tunachokizungumza ni kwamba kuna maeneo ambayo tunalazimika tutengeneze utaratibu wa kuweza kutoa muongozo mzuri kwa huduma za barabara, yaani watumiaji wa magari, vipando vya moto pamoja na watembea kwa miguu.

Maeneo ambayo barabara ziko mbovu tutaendelea kufanya jitihada zetu kuzijenga ili ziwe nzuri kama hapo awali. Maeneo ambayo yana makutano ya barabara ni lazima tuimarishe uwekaji wa taa ili kuweza kutoa mwangaza na muongozo mzuri kwa watumiaji wa barabara hizo.

Sasa nimuombe Mhe. Mshimba kwamba bajeti mbili hizi haziingiliani, tuliyotenga kwa ajili ya ku-*improve* barabara basi tutaendelea kufanya hivyo na tuliyoitenga kwa ajili ya uwekaji wa alama muhimu za barabara basi tutaendelea kufanya hivyo. Maana barabara bila ya alama haina tija, lazima uweke alama pamoja na hizi taa ili kuweza kutoa muongozo mzuri kwa watumiaji kuwakinga na ajali.

Nam. 63.

Ujenzi wa Barabara ya Mboriborini - Amani Fresh

Mhe. Fatma Mbarouk Said – Aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali katika utekelezaji wake imeahidi kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi na imeahidi kujenga barabara mbali mbali za Unguja na Pemba kikiwemo kijibarabara kidogo sana kushinda zote chenye kilomita moja kutoka Amani Fresh hadi Mboriborini. Na kwa kuwa sasa tuko kipindi cha lala salama kuelekea kwenye uchaguzi na bado kibarabara hicho hakijafikiriwa.

(a)Je, kwa nini kibarabara hicho ambacho kimekuwa kero kwa wananchi na hasa msimu wa mvua kisiwahiwe kujengwa haraka ili kisisahauliwe kutokana na udogo wake.

(b)Ni lini kibarabara hicho chenye kilomita chache kitajengwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 63 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara, imepewa majukumu ya kujenga na kuzifanyia matengenezo barabara zote zilizoainishwa kwenye sheria.

Aidha, Baraza la Manispaa la Mji wa Zanzibar pamoja na Halmashauri za Wilaya, pia zimepewa majukumu kwa mujibu wa sheria husika ya kuzifanyia matengenezo barabara zote za ndani zilizomo kwenye maeneo yao. Barabara anayoizungumzia Mhe Mwakilishi ni miongoni mwa barabara ambazo zinapaswa kusimamiwa na kutengenezwa na wenzetu wa Manispaa ya Mji wa Zanzibar. Lakini kwa kuzingatia kwamba Manispaa wana upungufu wa fedha. Sisi wizara yetu tuko tayari kutoa msaada wa vifaa na wataalamu, na wenzetu watusaidie gharama za mafuta ili tuweze kuinusuru.

Hata hivyo, kwa kipindi hiki wizara yetu bado tuna kazi nyingi za msingi za kufanya na tunamuomba Mhe. Mwakilishi atustahamilie.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa barabara iliyoulizwa katika swali la msingi inafanana na zile barabara za ndani zilizoko katika Jimbo langu la Mkwajuni. Kama anakumbuka Mhe. Naibu Waziri, tulishawahi kufanya ziara ya kutembelea kwenye barabara zile, tukapima na mambo mengine akaniambia wanakwenda kuzifanyia tathmini na baadae kutafuta uwezekano wa kuzijenga.

Mhe. Spika, nilikuwa nataka kujua tu, je, tathmini ile imekamilika na kama imekamilika ni lini zitakuja kujengwa.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe vijibarabara vya aina hii viko vingi katika majimbo mbali mbali. Hebu tushughulike na hichi kibarabara kilichotajwa sasa hivi. Mhe. Hamza Hassan Juma, swali lanyongeza, la mwisho hilo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwamtipura kuuliza swali la nyongeza kama hivi ifuatavyo. Mhe. Spika, barabara aliyoiuliza Mhe. Fatma Mbarouk Said Mwakilishi wa Jimbo la Amani, barabara hii imo ndani ya ilani

ya uchaguzi ya CCM na Mhe. Waziri alipokabidhiwa wizara, basi alikabidhiwa na ilani ya uchaguzi ya CCM.

Mhe. Spika, barabara hii tokea ilipoingizwa katika ilani ya CCM sasa hivi huu unakaribia mwaka wa 10. Je, Mhe. Waziri, haoni kutokuitengeneza barabara ile inayotoka Amani Fresh kupitia Mboriborini na vile vile kutoka Darajabovu mpaka Saateni ni kuidharau na kukiuka ilani ya uchaguzi ya CCM.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, mimi naamini Mhe. Hamza Hassan Juma ni mwenyeji sana katika Jimbo la Kwamtipura, Jimbo la Amani na maeneo ya ng'ambo na kwa msingi huo najua fika kafahamu barabara aliyoiuliza ya Mhe. Mwakilishi ni ipi, na hiyo barabara anayotaka kuchomekea ni ipi.

Mhe. Spika, sina kumbukumbu kichwani kama barabara anayoizungumza Mhe. Mwakilishi kwamba ni barabara moja. Barabara ambayo ameitaja Mhe. Hamza ya kutoka Darajabovu -Mboriborini mpaka Saateni, nakumbuka tulizungumza vizuri kwenye bajeti na tukakubaliana kuwa barabara hii imo katika PA. Sasa barabara aliyoizungumza Mhe. Fatma ni barabara nyengine, ingawa kuna pahala zinakutana, lakini ni vitu viwili tofauti.

Mhe. Spika, mimi kama mtu mwenye dhamana katika kumsaidia Mhe. Waziri, katika utekelezaji wa majukumu ya serikali bila shaka sote tunalazimika kutimiza wajibu na kuitekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi, hilo sina shaka nalo. Msingi hapa ni kwamba barabara aliyoizungumza Mhe. Mwakilishi katika swali la msingi, inatofautiana na barabara ambayo imekuja kuongezewa kuulizwa na Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Spika, majibu ni kwamba hii ambayo imekuja kuongezewa tayari tuna mpango nayo katika mpango wa PA, na madhumuni yetu ni kujenga. Hii ambayo imeulizwa leo, hili ni jukumu la wenzetu wa Manispaa na sisi kama wizara tuko tayari kutoa msaada wa vifaa na wataalamu na wenzetu wa Manispaa watusaidie gharama za mafuta na nyenginezo.

UTARATIBU

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kuhusu utaratibu ni kwamba Mhe. Naibu Waziri anasema kuwa barabara ambayo niliiulizia swali ni tofauti na hiyo barabara ambayo Mhe. Fatma Mbarouk aliyoiulizia.

Mhe. Spika, barabara hii sisi ndio tuliojenga hoja na hoja yetu Chama cha Mapinduzi kwa kuona uzito wake ndio ikaingiza katika ilani ya uchaguzi. Mhe. Spika, kama utaangalia kama sikosei ukurasa wa 127 kama hivi ya ilani

ya uchaguzi ambayo Mhe. Jaku Hashim Ayoub anayo pale, Mhe. Naibu Waziri, baadae nitamuonesha ili aone hiyo barabara yenyewe iliyokusudiwa.

Kwa hivyo, bado suala langu nilikuwa nakazia suala la Mhe. Fatma Mbarouk Said, kwa sababu majimbo yetu ni jirani na hiyo barabara ndio madhumuni yake. Kwa hivyo, nitamuomba Mhe. Spika, baadae Mhe. Naibu Waziri nikae nae ili tusome ile ilani ya uchaguzi nimuoneshe hiyo barabara yenyewe iliyokusudiwa. Ahsante.

Mhe. Spika: Ruhusa ya kukaa pamoja ipo, mnaweza mkakaa wakati wowote mtakaoona unafaa. Tunaendelea.

Nam. 47

Upanuzi wa Majengo ya Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Mhe. Spika, kabla sijajibiwa swali langu nambari 47, nataka nitowe pole kwa mwanafunzi Asha Hamad wa Pandani, baada ya kupewa dawa za Kichocho na Matende, baada ya macho yake kutoka nje na hivi sasa kichwa chake kinabonyea chote. Kutoka Pandani Pemba akaletwa Hospitali ya Mnazi Mmoja, hospitali ya rufaa na hapo ikashindikana na kupelekwa Muhimbili.

Baada ya maelezo hayo naomba wazee wastahamili na wawe pole.

Hospitali ya Mnazi Mmoja ambayo inategemewa sio muda mrefu kuitwa Hospitali ya Rufaa. Je, serikali haioni kuwa kuna umuhimu mkubwa sana wa kuvunja majengo yake ya zamani na kuyapanua ikiwemo Kitengo cha Macho cha Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri simama kwenye swali hili, sio yale maelezo yaliyotoka mwanzo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 47 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, wala hilo lisikushtuwe, mtoto ameshapimwa, anachuma cha ubongo ndio sababu iliyosababisha hilo na wala sio dawa za Kichocho na Matende.

Mhe. Spika: Endelea na swali.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, Hospitali ya Mnazi Mmoja ni Hospitali ya Rufaa kwa Zanzibar, na si kwamba inategemewa sio muda mrefu kuitwa Hospitali ya Rufaa. Kwani tukizungumza rufaa naomba tuelewe ni zile huduma maalumu zinazotolewa na hospitali ambazo hazitolewi na hospitali nyengine na si jengo lenyewe.

Mhe. Spika, haja ya kupanua Hospitali ya Mnazi Mmoja ipo, lakini si kuvunja majengo yake ya zamani na kuyapanua. Sababu ya msingi ni moja tu, kwamba Mnazi Mmoja ipo katika eneo la Mji Mkongwe na kwa Sheria ya Kimataifa *Stone Town* ni sehemu ya Urithi wa Dunia, unatakiwa kutunzwa kama ulivyo. Ndani ya jengo kunaweza kukafanywa mabadiliko. Kwa mfano, kukata vyumba ndani na kubadili vitu vinavyoharibika, lakini mabadiliko hayo yasiharibu uasili wa sura ya jengo lenyewe.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub:

(a) Mhe. Spika, sifa gani zinazotakiwa kuzingatiwa kabla ya hospitali kuitwa hospitali ya rufaa, ukizingatia majengo yetu yamekuwa machakavu, vipimo havipatikani kwa wakati hasa *CT Scan* na hata wakati mwengine hospitali hiyo kukosa maji.

(b) Majengo ya Mambo Msiige na majengo ya hospitali yepi yamo katika hifadhi ya Mji Mkongwe, wakati sheria ni moja tu ya uhifadhi wa Mji Mkongwe. Leo tunashuhudia hoteli kubwa inajengwa pale kwenye majengo ya Mambo Msiige. Je, ni sheria gani inayotumika pale na huku hospitali ya Mnazi Mmoja wananchi wanazidi kuteketea na sheria ni moja tu nchi hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, sisi tukitaka kufanya mabadiliko tunakwenda Mji Mkongwe kufanya mabadiliko watupe ruhusa. Tulitaka kujenga kijumba kidogo tu pale tuweke gesi wakatukatalia. Tulitaka tujenge bustani mbele ya Mnazi Mmoja kabla hatujatoa watu, wakasema hatuwezi tukabadilisha.

Kwa hivyo, sisi tunafuata tunavyoambiwa na Mji Mkongwe. Sheria ipi inatumika, kwa nini wengine wanapewa, kwa nini sisi hatupewi. Mimi sina taarifa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuweza kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali dogo tu la nyongeza kuweza

kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, pamoja na majibu yake mazuri kabisa yenye usikivu kwa wananchi wote waliokuwa wanatusikiliza.

Mhe. Naibu Waziri ulisema kuwa dhana ya kuitwa hospitali ya rufaa ni kwa kuwa kuna mambo ambayo ni muhimu yanapatikana pale. Je, Mhe. Naibu Waziri utakubaliana na mimi kwamba pakiwa na upungufu wa baadhi ya vifaa vya upimaji na kutokuvishughulikia, huoni kuwa unaondoa jina hilo la hospitali ya rufaa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, tunajipanga kuwa hospitali ya rufaa kwa vitendo. Wakati unapofanya hospitali ya rufaa unatakiwa uwe na huduma unazitowa. Lakini haina maana tena kwamba huduma hiyo ikipata tatizo imekuwa tena sio hospitali ya rufaa. Vitu vinanunuliwa, vinachakaa, na vinaharibika. Dawa zinanunuliwa na zinamalizika. Kinachotakiwa kuwe na pesa za kununulia nyengine, inapokosekana pesa kwa utaratibu unaokubalika inabidi huduma ile isimame mpaka tupate pesa. Sisi tunachokikusanya tunakipeleka serikalini na serikali inaturudishia. Huduma zikipanuka na gharama zikibadilika, vifaa vikipanda bei na kule sisi tunapungukiwa kwa sababu hata kile tulichokuwa tumekikadiria kinakuwa sio kile kilichoko nje.

Mhe. Spika, maisha kila siku yanabadilika. Ukinunua leo *reagent* kwa shilingi 10, ukienda kesho ni shilingi 30. Bajeti tuliipangia shilingi 10, pesa za mwaka mzima tunazitumia kwenye miezi mitatu. Sasa hiyo inaondosha dhana ya kuwa rufaa? Mimi sidhani! Huduma zipo, ikiwa hazitekelezeki kwa sababu ya upungufu fulani hilo ni jambo jengine.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa sababu hospitali yetu sasa hivi ni hospitali ya rufaa, je, hospitali ya rufaa inafanyakazi kwa muda gani, Kwa sababu unajua hospitali ya rufaa inafanyakazi kwa masaa 24. Lakini hivi karibuni tu nilikwenda na mgonjwa pale kiasi saa 3:00, daktari alishamuona kisha akamuandikia dawa, nikaambiwa niende kwenye chumba cha dawa. Mhe. Spika, ilipofika saa 3:00 madaktari wamejifungia na mafeni yao, nikagonga mpaka nikachoka, wasifunguwe kutoa dawa.

Mhe. Naibu Waziri: Mhe. Spika, hospitali ya Mnazi Mmoja inafanyakazi masaa 24. Sasa huyo kama hakuepo ni tatizo lake, atutajie siku na saa aliyokwenda tutafuatilia kwa sababu alikuwa anapaswa kuwepo kazini.

HOJA YA MJUMBE

(Hoja ya Mjumbe ya kuliomba Baraza la Wawakilishi Kutoa Azimio Dhidi ya Vitendo vya Udhalilishaji wa Watoto Zanzibar

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea tuna orodha ndefu kidogo ya wachangiaji wanaofika kama 9 na tunakusudia jioni tufunge mjadala huu. Kwa hivyo, tutumie muda mchache ili tuweze kuwakamilisha wote, lakini ni 10. Basi tuanze kumsikiliza Mhe. Asaa Othman Hamad, kwa kifupi sana na baadae Mhe. Salim Abdalla Hamad.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai, uzima na kuweza kuendelea na shughuli tulizotumwa na wananchi wa Zanzibar. Pili, nikushukuru wewe kwa kuniona.

Mhe. Spika, niungane na wale wote waliochukua nafasi nzuri ya kuichangia hotuba ya mjumbe wa Baraza lako tukufu Mhe. Mgeni Hassan Juma, iliyoliomba Baraza lako liridhie kwa kutungwa sheria dhidi ya udhalilishaji wa watoto.

Mhe. Spika, Wajumbe wako jana waliichangia hoja hii kwa kuonesha ni jinsi gani wanavyokerwa. Mhe. Spika, kwa sababu ni vitendo ambavyo kwa Zanzibar vinatoa mshangao mkubwa kwa Bara letu la Afrika.

Lakini pia, linaathiri vijana wetu wadogo kwa kiasi kikubwa. Baya zaidi ni jinsi hatua zinavyochukuliwa kwa vyombo vinavyohusika kutoa adhabu kwa wale wanaokutikana na hatia.

Mhe. Spika, jambo hili si tu kwamba wanaathirika vijana, lakini wanaathirika na wazazi, jamii, Taifa linapoteza nguvu kazi. Mhe. Spika, na leo naendelea tena kuwaomba sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kwamba wakati wa kunung'unika, na wakati wa kuvisikitikia vyombo hivi ambavyo ni kwa makusudi hatujui sababu, hawataki kuwajibika ipasavyo.

Mhe. Spika, sheria ziliopo dhidi ya wahalifu hawa wanaowadhalilisha watoto zinatoa mapungufu makubwa, visingizio kule polisi na hata Mahakamani kwenyewe ni kukosekana ushahidi wa kuwatia hatiani wale wanaokutwa na balaa hili. Nadhani ni wakati muafaka sasa, Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuchukua hatua muafaka za kuwasilisha Mswada wa Sheria, na Baraza lako Wajumbe waweze kuipitisha sheria hiyo. Sheria ambayo itafunika ile mianya

inayotumiwa sasa. Sheria ambayo itazuia vyombo vinavyolalamikiwa kwamba kwa makusudi havitendi haki kwa kushingizia visingizio vya ushahidi.

Mhe. Spika, lawama kubwa imetupiwa jeshi letu la Polisi, lakini pia kukatajwa na Mahakama zenyewe. Lakini tatu baadhi ya watu ambao huwa hawataki kwa makusudi kutoa ushahidi kwenye vyombo hivi. Kulitolewa ushahidi mbali mbali ulitajwa hata jana na Wajumbe jinsi gani udhalilishaji huo wa watoto wadogo unavyoongezeka siku hadi siku. Lililowaliza Wajumbe kwa bahati mbaya hata kuna wazazi wanawatendea vitendo hivi watoto waliowazaa. Mhe. Spika, hili ni jambo gumu sana tena baya, ni vitendo vya aibu!

Mhe. Spika, hivi vitendo hivi leo vinashamiri Zanzibar hii na wenzetu wanaoifahamu Zanzibar kweli hatuna nyuso mbele ya wenzetu, tukubali tufanye jambo ambalo litarejesha heshima ya visiwa hivi, na jambo ni kuweka sheria itakayofunika mianya ile inayotoa visingizio vya kukosekana ushahidi, ili kuondoa malalamiko kwa chombo cha polisi, mahakama na kwengineko.

Ningewaomba wenzangu wa Baraza hili kikao kinachokuja kama hili tunalichukia wala tusichukie kwa kusema, tuchukie kwa kutenda. Tulete Mswada hapa wa kupendekeza sheria tuugawanye maeneo matatu mazuri kwa yule mzazi atakayetiwa hatiani kumdhalilisha mtoto ama kumlawiti huyu ni viboko 50 hadharani kwanza na la pili anyongwe. Lakini ukimuacha mzazi kwa wale wengine wao ni kumnyonga hakuna lugha nyengine.

Nafahamu Mhe. Spika, ukiitaja lugha hii kuna wenzetu watakuja na malalamiko ya kusingizia haki za binaadamu. Lakini jibu sisi tunalo kwamba na hivi vitendo sivyo vya binaadamu. Binaadamu hatendi kitendo hiki kwa binaadamu mwenziwe. Kwa hiyo, hatuwezi kujilabu kwamba tunavunja haki za binaadamu kumbe huyu siye binaadamu.

Mhe. Spika, inapofika mahali binaadamu kwa sura akatenda vitendo anavyovifanya mnyama na ukamfananisha na yule mnyama binaadamu huyu, sasa inakuwa unamdhalilisha yule mnyama sana. Huyu ana fungu jengine, huyu si binaadamu wala si mnyama, mtafutie fungu lake umuweke. Ndio nasema sheria ya mtu kama huyu ni kumnyonga. Huyu keshaua, kamuua kimaisha huyu kijana, keshaua ndani ya familia, jamii hii keshaiweka mahali pabaya lakini taifa linaendelea kumong'onyoka na vijana wanapotea.

Mhe. Spika, udhalilishaji wa namna hii unaathiri mpaka kisaikolojia kwa mama ambaye mtoto wake katendewa kitendo hiki, Mheshimiwa hana uso hata wa kutoka nje, hawezi tena huyu mama kuhudhuria kwenye hafla zozote

za kijamii. Wenzake wakimtizama yeye anaumia, watu wakicheka yeye anafikiria anachekwa yeye, wakinong'ona ni hivyo hivyo, kwa nini tuendelee kuwabembeleza watu wa namna hii na kuendeleza maovu.

Mhe. Spika, Zanzibar ina wazanzibari wanaoamini dini zao. Serikali haina dini, walio wengi Zanzibar wana dini kubwa tunayoiamini, haya hayakubaliki. Kwa sababu dini yetu sisi Wazanzibari haya hawayakubali na sisi ndio wenye maamuzi kuyakataa na serikali lazima itukubali sisi. Sisi katika hili wanaozungumza haki za binaadamu nadhani watakubaliana na sisi kwamba haki za binaadamu watoto wa Kizanzibari zinavunjwa, na kama zinavunjwa Wazanzibari ni lazima wakatae na wazilinde kwa namna yoyote ile.

Mhe. Spika, mzazi anapofika kumlawiti mtoto aliyemzaa mwenyewe au kaka au mjomba au ndugu aliyezaliwa naye mwenyewe. Mhe. Spika, katika hili si suala la kulipa nafasi tena kwa muda uliofika na kwa hali inayoendelea kwa kasi kubwa, ni lazima serikali itukubalie jamii hii iliyoamua maovu haya wachukuliwe hatua muafaka ya kukomesha na sio kupunguza, sifa hii hatuitaki itajwe katika visiwa hivi.

Mhe. Spika, kulitajwa jengine ambalo mzazi aliyembaka mtoto wake, kesi ikapelekwa lakini hatimaye baba na mama na yule mtoto. Mtoto ni mtoto wamekaa naye, wamembembeleza, wakaenda polisi kwamba huyu mzazi aliyetenda kitendo hiki kwamba amesamehewa na yule mtoto kwa kumtafutia shilingi laki tano na mama mtu na yeye alikubali.

Nasema Waheshimiwa Wajumbe na kwa wale mama watakaoshirikiana na waume zao kuficha ukweli huu, au na yeye akaunga mkono kwamba mumewe asitiwe hatiani, huyu mama yake iwe ni miaka kumi. Kama mama amemzaa mtoto, baba mtu akaweza kumlawiti mtoto huyu au kumbaka na mama eti kwa kumlinda mumewe anafika mbele ya sheria anasema kwamba kamsamehe mume. Sijui atakaa naye vipi mume kama huyu. Sijui atakaa naye vipi hapa nyumbani kwao.

Waheshimiwa Wajumbe nadhani katika sheria ambayo tutake Mswada huo kuutengeneza mama wa namna hii ni miaka kumi, mume viboko hamsini na kunyongwa, jengine halipo. Tuone yatakoma au yataendelea. Mhe. Spika, kesi 74 zilizochukuliwa hatua ni 2, kesi 48 hatua zimechukuliwa ni kesi 2, 38 hatua zilizochukuliwa ni kesi 2 maana ndiyo kawaida sasa ni 2, zikiwa 100 ni 2, zikiwa 1000 ni 2. Ndizo zinazopatikana ushahidi, hivi ni kweli.

Ushahidi Mhe. Spika, ni wa kuona. Unamuona huyu kijana kaathirika, maumbile yake siyo aliyoumbwa na Mwenyezi Mungu huyu bwana

keshayabadilisha. Tunataka ushahidi upi mwengine. Lakini ushahidi mwengine hapa duniani ni daktari kathibitisha huyu kaathirika. Daktari yeye aliyemuathiri hakumuona, lakini kwa kutumia vipimo vyake anatuthibitishia kamba huyu kaathirika na sisi waja wengine tusio na vyombo macho yanatwambia huyu kaathirika. Na mtoto anasema kwamba huyu ndiye aliyeniathiri. Hili halafu tunasema ushahidi hautoshi, tunataka ushahidi kutoka wapi sasa. Hizi ndio sheria ambazo zimetoa mianya ya kuwapa wenzetu nafasi kuendelea na maovu haya.

Waheshimiwa Wajumbe nafasi ni yetu, maovu haya wanafanyiwa watoto wetu, sasa ni kuleta Mswada wa sheria tuyakomeshe haya na tuache kuinung'unikia serikali, polisi, wala Mahakama. Mhe. Spika, nakushukuru ahsante.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, na mimi naungana na wenzengu kutoa shukurani kwa kupata nafasi ya kuchangia hoja hii ya Mhe. Mjumbe mwenzetu wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Mgeni Hassan Juma ya kutoa maazimio dhidi ya vitendo vya udhalilishaji wa watoto Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi kwanza nitoe shukurani za dhati na nimpongeze Mjumbe mwenzetu wa Baraza hili la Wawakilishi kukaa, kufikiri, kuchunguza, kutafakari na hatimaye akaamua kuleta azimio hili. Hakulileta kwa bahati mbaya tu, lakini pia kalileta kutokana na kuwa ni lenye kumuumiza katika moyo ikiwa ni mzazi, na hivyo hivyo ndivyo tulivyo na sisi kwa ushahidi Mhe. Spika, hata juzi tulipokuwepo katika *briefing*, alitoa malalamiko yake kwa vyombo vya habari, kueleza kuwa hizi *channel* zilizoingizwa safari hii na hasa baada ya kupata mfumo huu wa *digital*, unaathiri sana silka, mila, utamaduni, desturi za watoto wetu na zinawapeleka kule ambako sipo.

Alitoa ushauri kama uwezekano upo wa kushughulikiwa ishughulikiwe ili hali hii ipungue. Mimi nilisikitika sana kweli kweli kwa jambo muhimu kama hili akapewa jibu kuwa hii ni dijitali haigusi kwamba mtu aangalie wapi atizame na wapi asitizame, wakati mwenye kutoa jibu hili ni Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, na utamaduni wetu tunao wa aina yetu na tunapoona kuwa unakwenda kinyume na utamaduni wetu ni wajibu wetu kulizungumza suala ni muhimu sana. Lakini nashukuru kabla kwa busara zako kuwa ulielekeza kuwa hili suala lishughulikiwe.

Mhe. Spika, tunajua kila kinachozaa mtoto wake huwa anahitaji malezi maalum, inatofautiana baina ya viumbe na viumbe. Hata kuku anapokuwa na watoto wake anawalea, anawaelekeza na anawalinda. Viumbe wengine ili watoto wawe wazuri, wawe na kinga, waweze kukua inavyofaa, Mwenyezi Mungu kawajaalia wazazi wao kawapa maziwa wananyonya, na

wanawasaidia kwa kila kitu. Halafu kuna mambo mengine ya kumlea yule mtoto aelekee lile ni jukumu la wazazi sote. Kwa bahati mbaya tukiangalia hivi sasa tulivyo na tukiangalia huko tunakotoka sisi wakati ni watoto wadogo kuna tofauti kubwa sana. Hivi sasa usasa unatupeleka mahali pabaya sana.

Tujue tukizungumza mtoto maana yake ni mtoto, ni mwepesi wa kuiga jambo liwe zuri au liwe baya. Tukitembea mitaani hivi sasa Mhe. Spika, tunawakuta watoto wetu tena ni wanaume wa kuwategemea lakini wanateremsha suruali mpaka hapa chini, maana yake nini. Hawaulizwi, hawashughulikiwi tunasema tunakwenda na wakati, matokeo yake watoto wetu wanaingia katika hali ya kudhalilishwa kiasi ambacho ni cha kutisha mpaka Mheshimiwa ikabidi alete azimio hili.

Mhe. Spika, tukiangalia katika karatasi yake aliyoileta kwanza namshukuru kwa utafiti alioufanya kwa muda wa miaka mitatu; mwaka 2010, 2011 na 2012. Katika utafiti wake na kulingana na aina kadhaa za udhalilishaji, Mheshimiwa amegundua jumla ya watu 156 kwa miaka hii mitatu walifunguliwa kesi za udhalilishaji na kenda mbali zaidi, kazitafautisha ile aina ya udhalilishaji kama ifuatavyo. Kuna wale ambao wana kesi za udhalilishaji wa kufanya mambo kinyume na maumbile. Nikisema hivyo nafikiri nafahamika.

Hawa kwa miaka mitatu kakusanya jumla ya watoto 28. Hii ni mbaya sana. Kuna wale ambao wamebakwa kapata jumla ya watu 118. Kuna wale ambao kesi zao zilimalizia kulipa faini amepata watu 10. Katika kesi 156 ni 10 tu ndio waliohukumiwa kulipa faini.

Kuna wale ambao wameachwa huru kabisa kuwa hawana makosa ni 68, kuna kesi zinazoendelea ni 112. Halafu kuna wale ambao hawa wanaonekana wana makosa na hawa wakahukumiwa kifungo, katika jumla ya watu 156 ni watu 6 tu kila mwaka ni watu wawili. Huu ni utafiti kwa watu wanaopelekwa Mahakamani kwa udhalilishaji, lakini naamini kuna makundi na makundi ya watu katika mazingira tofauti ya udhalilishaji yanaendelea na bahati mbaya hayapelekwi Mahakamani.

Sasa Mheshimiwa mtu kama atapeleka kesi Mahakamani hii ni kesi ya aibu, na kwa Wazanzibari kutokana na mila na desturi zetu tulizonazo na silka zetu hatupendi kupeleka aibu Mahakamani, lakini mpaka ikipelekwa huwa haina budi. Leo katika watu 156 watu 68 wanaambiwa nyinyi mko huru na hamna makosa na kuna kesi mpaka leo zinaendelea 112, lakini 6 tu ndio waliopewa hukumu za kufungwa. Hatuingilii Mahakama lakini ukiangalia kesi zilivyo ni za watoto, za aibu za kutisha zikapelekwa Mahakamani katika kundi lote hilo wakabainika 6 tu ndio wenye makosa na wakahukumiwa kifungo.

Mhe. Spika, sina uhakika lakini mimi natia mashaka kuwa haki haitendeki ipasavyo huko watoto wetu wanakopelekwa. Kama serikali haikuwa *serious* ikaonekana kama mtu kafanywa kitendo halafu huna ushahidi halafu ikachukuliwa hukumu tena ambayo ni ya kutisha watu wakaogopa, kwa namna hii Mheshimiwa sisi ndio walezi, watoto wanakokwenda huko tutakuja kuona tuna taifa la watu ambao hawatambuliki wakoje, ni hatari inatuelekea. Kwa maana hiyo naunga mkono kikamilifu na azimio alilotoa Mhe. Mgeni Hassan Juma hasa azimio Nam. 4.

> "Kutokana na udhaifu unaoonekana katika kushughulikia kesi za udhalilishaji watoto. Kwa hivyo, serikali ianze utaratibu wa mafunzo ya pamoja ndani na nje ya nchi katika vipindi maalum kwa wahusika wanaosimamia mfumo wa utoaji haki katika kesi za watoto wakiwemo Mahakimu, waendeshaji wa mashtaka, polisi, madaktari, Makarani na wengi wengineo ili ionekane kuwa haki inatendeka vilivyo"

Jengine, kuna suala Mheshimiwa kapendekeza serikali ione umuhimu wa suala hili na kwa vyovyote itakavyokuwa hichi kifaa kinachokosekana cha *DNA* kinapatikana haraka ili hukumu iweze kutoka kwa haraka. Lakini najua serikali ikitaka itafanya na hili si suala kwamba serikali imeweka azimio ni kutafuta njia kutekeleza tu, kwa sababu kuna mengi mazito serikali inatekeleza kuliko haya yanatekelezwa bila ya kutafutwa azimio. Lakini kuna mambo yanaendelea ya mtu kukamatwa *red-handed* hii haitaki *DNA*, hataki lolote isipokuwa ni ushahidi uliokuwa hauna matatizo. Leo watoto wetu masikini wanadhalilishwa, wanaonewa, na kesi inavyokwenda Mahakamani inachukua muda mrefu mpaka mzee anayemshughulikia yule mtoto hawezi kujieleza ipasavyo. Inabidi aachie njiani na maana yake huwa kesi kumalizika.

Mimi binafsi nikiwa Mwakilishi wa Jimbo la Mtambwe nimepata kesi nyingi za aina hii, nimeziona haziendi vizuri kwa kule Pemba nikampa taarifa Afisa Mdhamini anayeshughulikia hii Wizara, nimpongeze anajitahidi sana kufuatilia lakini mwisho tunaona mambo ni kimya. Kwa hivyo, kuna pazia baina ya haki na watoto wanaodhalilishwa. Tunaiomba serikali itupie darubini ione kuwa popote ambapo haki haitendeki wakati hii ni muadhara mkubwa kwa watoto wetu pamoja na hasara ya taifa kwa hivyo inashughulikiwa vilivyo.

Mhe. Spika, hata juzi katika jimbo langu nimeambiwa na Waheshimiwa mpaka leo nina unyonge, mtoto wa miaka minne tu lakini kaharibiwa na baro baro la miaka 20, hii ni hatari. Sasa ikishakuwa Zanzibar hii inafika hivi kwa yale yanayojulikana na mengine mengi hayajulikani, basi tujue Mheshimiwa tupo katika mahala pa hatari na ni lazima hili suala lishughulikiwe ipasavyo.

Mwisho kwa vile muda umekwisha naiomba kwa heshima zote tena naiomba *seriously* Wizara yetu ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, ione kuwa ina wajibu mkubwa sana wa kusaidia katika kupunguza suala hili kwa kuchukua vipindi vya kuelimisha, na kwa kutumia wataalamu wa aina zote, ikiwa ni polisi, ikiwa ni mashekhe, wanasheria na kadhalika. Pia, kwa kuona kuwa huu utamaduni unaotupelekea mpaka watu ikawa wanaingia katika mambo yaliyokuwa hayastahiki hauna lazima ukauachia ukaendelea.

Umefika wakati Mhe. Spika, tuangalie sana vipindi vyetu vya televisheni na hao wanaojiajiri katika kutuonesha mambo kadhaa, Wizara itoe ushauri kwa kuonesha yale mambo ambayo yana maslahi nasi, tufuate malezi yetu ya kizamani ili taifa hili liokoke. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi kutoa maoni yangu angalau madogo kuhusu maazimio ya Mhe. Mgeni Hassan Juma.

Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba nimpongeze kwa dhati kabisa Mhe. Mgeni Hassan Juma, kwa kuamua kwa makusudi kuleta hoja hii mbele ya Baraza lako Tukufu, hoja ya maazimio dhidi ya vitendo vya udhalilishaji wa watoto Zanzibar.

Mhe. Spika, Mhe. Mgeni Hassan Juma, ameonesha hisia zake jinsi gani anavyoumwa na anavyoumia na kufikia kuleta hoja hii inayoonesha kuwepo kwa ongezeko kubwa la udhalilishaji wa aina mbali mbali na jinsi kesi zake zinavyokwenda na zinavyoishia bila ya hukumu muafaka.

Mhe. Spika, Mhe. Mgeni Hassan Juma, ametoa takwimu ambazo wenzangu wengi wameshazieleza, takwimu hizi ambazo zimeripotiwa tu lakini naamini kwamba kuna matukio mengi ambayo yanatokea lakini matukio hayo hayaripotiwi. Ima yanaishia polisi, ama yanaishia majumbani. Kwa hivyo, inawezekana kuna matukio makubwa yanatokea lakini matukio hayo mwisho wake inakuwa yanaishia hivi hivi.

Mhe. Spika, leo katika redio kwenye kipindi cha mawio zimetolewa taarifa hizi za udhalilishaji wa watoto kijinsia ni taarifa za kusikitisha, taarifa ambazo zipo wazi hazihitaji ushahidi wa ziada. Lakini matokeo yake kesi zile zimekwenda hivi hivi. Inavyoonekana kwamba tatizo kubwa ambalo linaathiri ni jeshi la polisi hili linasaidia kwa kiasi kikubwa kusababisha kesi hizi zisiende, na matokeo yake kutolewa hukumu ambazo hazistahiki.

Mhe. Spika, sitaki kuchukua muda wako mrefu, lakini na mimi nimeona kwa sababu na mimi ni mama na mimi nina watoto na mimi nimeguswa kwa kiasi

fulani na tatizo hili. Na mimi nimeona nitoe angalau maelezo yangu mafupi halafu niunge mkono. Naunga mkono maazimio tisa yote ya Mhe. Mgeni Hassan Juma, kwa asilimia 100. Ni maazimio mazuri, nimeona nikikaa kimya itakuwa sio vizuri, kwa hivyo Mhe. Spika, katika maazimio haya naomba nitilie mkazo baadhi ya maazimio.

Kwanza kabisa Mhe. Spika, naomba nitilie mkazo azimio namba 2, la Mhe. Mgeni azimio ambalo ameomba kwamba bajeti ya serikali ya mwaka 2014/2015 na zinazofuata ziweke mkakati wa kupambana na suala hili. Mhe. Spika, mimi ninalitilia mkazo hili na naomba serikali katika bajeti yake iweke mikakati ya kuweka kipaumbele suala hili la udhalilishaji wa watoto kijinsia.

Halafu Mhe. Spika, katika kipengele cha 4 cha maazimio ya Mhe. Mgeni na hiki nacho Mhe. Spika, naomba nacho nikitilie mkazo. Kuhusu *coordination*, Mhe. Spika, kinachotukwaza ni kwamba kunakuwa hakuna *coordination* nzuri baina ya hizi taasisi ambazo zinashughulikia masuala haya. Daktari akitoa ushahidi Polisi anaubadilisha ushahidi, Polisi akitoa ushahidi mahkama na hapa Mhe. Spika, kinachoonekana kinachotukwaza zaidi ni rushwa, Mtu anajali ile senti ambayo atapewa ataitumia siku mbili hajali maisha ya yule mtoto ambaye amedhalilishwa na ambaye amepotozewa muelekeo wa maisha yake.

Naomba Mhe. Spika, serikali ipange kwa makusudi itufanyie semina sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pamoja na mihimili yote hii tukae kwa pamoja tusemane, tuelekezane, ifikie wakati hizi kesi zinavyokwenda ziende kwa vizuri.

Mhe. Spika, jengine ni kipengele cha 5 kuhusu serikali iingize mitaala ya elimu katika maskuli, Mhe. Spika, hili naliunga mkono asilimia 100 ikiwezekana na 50 kwa sababu Mhe, watoto wakati mwengine mtoto anaweza kumsikiliza mwalimu zaidi kuliko hata mzee wake. Kwa hivyo, Mhe. Spika, hili tukiliweka likianza kutolewa maelekezo maskulini likiwa ni somo maalumu la kufahamishwa watoto kwamba kuna tatizo hili na hili. Kwa hivyo, ukiambiwa hivi ufanye hivi au toa ripoti kaseme kwenu, kaseme Polisi nadhani litaleta mafanikio mazuri katika suala hili na pengine labda litapunguza ile idadi ya kesi na itapunguza masuala hayo ya udhalilishaji kwa watoto.

Mhe. Spika, jengine la mwisho ambalo ninalitilia mkazo ni azimio la 8 Mhe. Mgeni, ameeleza kwamba ili kurahisisha upelelezi wa kesi za udhalilishaji wa watoto kuhusu *DNA.* Mhe. Spika, *DNA* imekuwa kama wimbo wa taifa katika Baraza hili, yaani wakati wa bajeti mambo mengi tu *DNA*, lakini inaonekana kwamba serikali bado haijawa tayari kuhusu utafutaji wa hii *DNA* na *DNA*

ndio ambayo itakayotatua matatizo haya kwa sababu hii ndio itakayotoa ushahidi kamili kuhusu masuala haya ya udhalilishaji.

Mhe. Spika, ninachokiomba kama serikali ilivyoamua kwa makusudi kukata bajeti za Wizara zote kununuliwa meli kutokana na majanga ya meli yaliyotokea. Naomba serikali na kwa makusudi ikate bajeti za Wizara zote ili kupatikana hii mashine ya *DNA* ili suala hili liweze kupatiwa ufumbuzi. Mhe. Spika, mimi sidhani kama serikali ikikusudia inashindwa kufanya hivyo mimi naomba iwe hivyo.

Mhe. Spika, pia pamoja na hayo pia niunge mkono Mhe. Hija alipotoa maelezo yake aliongezea vitu vitatu lakini mimi katika vitu hivyo kimoja cha utamaduni wa mavazi nakitoa kwa sababu Mhe. Spika, hawa wadhalilishaji wanakuwa wanawabaka hata watoto wa miezi hata mwaka hawajafika. Sidhani kwamba yule atakuwa kafanya vile kwa sababu kapenda vazi lake alivyovalishwa sidhani.Kwa hivyo, mimi sifikirii kama labda mavazi yanaweza kuchangia hilo. Mimi nadhani wanakuwa tu tayari anakuwa nao mbakaji kama huyu.

Kwa hivyo, naunga mkono maazimio ya Mhe. Hija Hassan Hija, moja kwamba wale wabakaji wasifichwe, waanze kutajwa hadharani pale mwanzo tu ambapo linapoanza suala hili. Kesi iko Polisi kabla haijenda mahkamani basi vyombo vya habari vitumiwe kumtangaza yule ianze pale. Kwa hivyo, naliunga mkono azimio la Mhe. Hija Hassan Hija, alilioliongeza kwamba wabakaji watajwe hadharani.

Vile vile, naunga mkono nyongeza ya Mhe. Hija Hassan Hija, ya kwamba hawa vitangi hawa jina la mwanzo walipoanza hawa wabakaji jina la mwanzo ilikuwa wanaitwa *vitangi*, hawa vitangi sugu Mhe. Spika, naomba azimio lipitishwe hapa wahasiwe. Mimi nadhani hawa wakihasiwa watafanya nini tena. Kwa hivyo, naomba kuunga mkono hilo ambalo Mhe. Hija Hassan Hija, kaliongeza.

Mhe. Spika, sitaki kuchukua muda wako mrefu, mengi sana wameshasema wenzangu, mengine yameshachangiwa. Kwa hivyo, Mhe. Spika, kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kusini, naunga mkono maazimio ya Mhe. Mgeni asilimia mia moja. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya, kwa kunijaalia uzima wa kuweza kusimama hapa mbele ya Baraza lako hili nikiwa mzima na afya njema. Lakini pia nichukue fursa hii ya dhati kabisa Mhe. Spika, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niwe mchangiaji kwenye hoja hii

ambayo ni muhimu sana kwa maslahi ya watoto wetu na kwa maslahi ya taifa letu.

Pili, Mhe. Spika, nichukue nafasi hii pia ya dhati kabisa ambayo inatoka ndani ya moyo wangu, ndani ya sakafu ya moyo wangu, nimshukuru na kumpongeza Mhe. Mgeni Hassan Juma, mtoa hoja binafsi. Mhe. Spika, lazima tukubali kwamba hoja ni ya msingi lakini hoja hii kwa kweli inatugusa sote humu ndani na walio nje. Sote inatuuma ndani ya mioyo wetu, sote inatutia *pressure* lakini Mhe. Mgeni ame- *feel*, ame-*respond* na akaamua kuleta hoja hii binafsi.

Kwa kweli Mhe. Mgeni Hassan Juma, tunakupongeza kwa ujasiri wako huu mkubwa wa kuleta hoja hii ambayo muhimu sana, na tunaamini kwamba Baraza lako hili tukufu Waheshimiwa wanawake labda niseme kwa asilimia 70 sote tukimaliza hoja hii basi tutakuwa tumechangia hoja hii ya msingi, lakini sisi kama kinamama kama wazazi, ambao ndio tunaokwenda *labour* kwa kweli yanatuuma sana matendo haya.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa hoja ya Mhe. Mgeni inaonekana kwamba taarifa zinaonesha kwamba kwa mwaka wanafanyiwa matendo haya watoto 70 Mhe. Spika, ni hatari kubwa. Kwa sababu nchi yetu ni visiwa viwili, watu kidogo ikiwa kila mwaka matendo haya yanaongezeka inaonekana kwamba itafikia kila mwaka wanaweza wakafanyiwa matendo haya ya udhalilishaji mia na yataendelea.

Kwa hivyo, sasa kama serikali haijakaa ikaunda mbinu madhubuti kwa kweli matendo haya yataongezeka siku hadi siku. Mhe. Spika, tujiulize kwa nini matendo haya yanaongezeka siku hadi siku. Inaonekana kwamba sheria yetu hii bado ina udhaifu, kwa lugha nyengine pengine haina meno madhubuti ndio maana matendo haya yanaongezeka. Na ndio maana wafanyaji wa matendo haya hawaogopi.

Lakini kabla sijaingia katika hoja hii Mhe. Spika, niombe kwamba hoja ya Mhe. Mgeni kwa kusema marekebisho haya yafanyike basi kwanza hao wanaoshutumiwa kuwa wamefanya matendo haya wasichukuliwe dhamana. Kwa sababu wanapochukuliwa dhamana hatujui kule nje wanafanya nini, lakini pia wanajisifu, inaonekana kwamba hakuna hatua inayofanyika. Lakini pia wanafanya uenyeji mkubwa kuona kwamba kesi hizi zinafifia.

Mhe. Spika, Mhe, mtoa hoja amezungumza mambo tofauti humu katika hoja yake kuonesha kwamba bado hali si nzuri katika udhalilishaji wa watoto wetu.

Nije mimi katika hoja namba 4 Mhe. Spika, jinsi ya ushughulikiaji wa kesi hizi za ubakaji. Mhe. Spika, hivi karibuni kama mwezi ilitokea mtoto wa miaka 9 amebakwa na kesi iliendeshwa katika mahkama ya Mwera, Mhe. Waziri naomba hili suala alishughulikie. Cha kusikitisha hakimu alikuwa ni mwanamke ambaye ni mzazi, mimi ninaamini kwamba mwanamke anaumia zaidi kuliko mwanamme.

Mhe. Spika: Hiyo kesi inaendelea au...

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Imeshatolewa hukumu. Kwa hivyo, ile kesi ilionekana kweli mbakaji amefanya tendo hilo, mbakaji ana umri kama wa miaka 27,28, au 29 lakini hatimae hakimu akatoa hukumu kwamba mbakaji atoe faini ya laki nne. Laki tatu ziingie katika mfuko wa serikali lakini laki moja wapewe wazee wa familia iwe ndio kifuta jasho chao. Mhe. Spika, hivi tujiulize kweli laki moja inaweza ikamlipa mtoto yule aliyebakwa. *Is it fair*, Mhe. Spika, Inasikitisha, inatuuma. Kwa hivyo inaonekana dhahiri kama katika mahkama zetu chembe ya rushwa ipo, sasa kweli Mhe. Spika, tutamaliza masuala haya. Hatuwezi kumaliza.

Mimi nimuombe Mhe. Waziri kwa sababu kesi imefanyika kama mwezi tu sasa hivi lifuatilie hilo suala na kesi ikiwezekana ifanyike tena Mhe. Spika, hatujamtendea haki huyu mtoto laki moja, ameshaharibiwa kila kitu. Kuna watoto wanabakwa kwa kweli mpaka akili yake inakuwa si nzuri kila wakati anamuota yule aliyembaka. Wako watoto wanaweweseka humu tumeshapata kesi hizo baba ananijia, mama ananijia! Mhe. Spika, kwa kweli hali si nzuri huko nje.

Mhe. Spika, nikiendelea katika hoja hii kwa sababu wengi wameshachangia nije katika suala la *DNA*. Mhe. Spika, mimi nimpongeze Mhe. Mgeni kwa hoja hii ya kununua kifaa hiki cha *DNA*. Mhe. Spika, wewe ni shahidi tushazungumza sana katika kununua kifaa hiki lakini mimi naamini serikali inaweza. Hivi karibuni imeamua kununua meli na ikabana bajeti za Wizara zote na hatimaye tunaletewa taarifa kwamba meli imo katika *process*. Kwa hivyo, naomba serikali, serikali na wao binaadamu na wao wazazi kwa kweli tuwaonee huruma watoto wetu, kifaa hiki mimi nimuunge mkono Mhe. Mgeni Hassan Juma, bajeti itakayokuja lazima Wizara husika ituletee hapa taarifa kwamba bajeti pesa hizi zimeshatengwa kwa ajili ya kununua kifaa hiki cha *DNA.*

Mhe. Spika, nasema hivi kwa sababu huwezi kumtambua aliyefanya tukio hili kwa macho na wale si wendawazimu wana akili timamu, mbona hawafanyi hadharani wanatafuta wasaa muafaka wanafanya matendo haya. Kwa hivyo,

pekee kitachotusaidia katika kumtambua mfanyaji wa tendo hili ni kifaa hiki cha *DNA.*

Wenzetu nchi zilizoendelea kwa kweli ndicho kifaa ambacho kinawasaidia na ndio maana matendo haya kwa wenzetu yamepungua si mengi, na kama yanafanyika kwamba mtuhumiwa atajulikana na atapatikana atachukuliwa hatua. Lakini kama sisi tutakaa hapa tutasema kila siku, tutapiga kelele, tutaumia vifua lakini kama kifaa hiki cha *DNA* hakijanunuliwa, tatizo hili hatuwezi kulitatua.

Mhe. Spika, mbali ya tukio hili la ubakaji la watoto kuna matukio mengine mapya yamezuka. Sasa hivi Mhe. Spika, kwa taarifa yako tu kama utakwenda hospitali ya Mnazi Mmoja wanapokea watoto chini ya miaka 18 waliotiwa mimba, kwa mwezi wanapokea watoto kuanzia 15 mpaka 20, *wallahi* Mhe. Spika, nakwambia, watoto wale ni wanafunzi, wadogo, lakini kesi hizi zinapokwenda Polisi, Polisi hazina ushahidi utamtambuaje mtu aliyetia mimba kama huna kifaa cha *DNA*, bila shaka mtoto yule ajifungue, mtoto apimwe damu ile aonekane mtu ambaye amefanya tukio hilo.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kwa taarifa yako tu ni hatari kubwa tunayokwenda nayo. Kwa sababu fikiria Mhe. Spika, kama itakuwa kwa mwezi watoto 15 mpaka 20 wanaotiwa mimba za utotoni ambao watoto hao hawajatimia hata miaka 18, kwa mwaka watoto wangapi tutapata ambao wana mimba za utotoni.

Kwa hivyo, mimi nimuombe Mhe. Waziri niiombe serikali kifaa hiki mwakani ikifika iwe tayari tushapata ufumbuzi wa ununuzi wa kifaa hiki. Tunaumia sisi ndio wazazi Mhe. Spika, inatuuma inatupandisha *pressure*, kuna wazazi hawajaunga humu mpaka leo kwa watoto wao kufanyiwa mambo haya. Aidha mtoto mdogo katiwa mimba au mtoto wake mdogo amebakwa.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nije suala zima la jamii, lazima jamii nayo ikubali kusaidia suala hili si serikali tu peke yake, kwa sababu wapo watu ambao wanafanya matendo haya katika jamii aidha jirani au mwanafamilia. Lakini hatimaye wanafamilia wale wameshamgundua mtu amefanya kama baba au mjomba au kaka lakini mwisho wake wa kesi wanafamilia wanasema oo maana yake tumeshakaa wanafamilia pengine baba ameamua kumlipa mtoto huyu laki tano hivi kweli mtoto tunamdhalilisha. Mtoto naye ana haki yake ya msingi pamoja na kuwa wewe mzazi umemzaa mtoto yule wako, lakini bado mtoto naye ana haki yake ya kimsingi katika suala lile.

Kwa hivyo, mimi nimuombe Mhe. Mgeni atakapokuja ku-*wind up* aitie kwamba marekebisho haya ya sheria yaingizwe kwamba mzee naye yeyote akipatikana kwamba na yeye kajiingiza katika suala hili kuwa amesema wazee wameshakaa, washaamua kuwa asamehewe atamlipa mtoto huyu na yeye achukuliwe hatua. Na yeye afungwe japo miaka 5 au 3 inawezekana ikasaidia kupunguza matukio hayo, lakini kama si hivyo hayawezi kupungua. Kwa sababu inaonekana kwamba jamii nayo ina ufahamu mdogo na haitusaidii katika suala hili.

Lakini pia, Mhe. Spika, nije katika baadhi ya Mikoa mtoto akishafanyiwa suala lile la ubakaji pengine mtoto wa miaka 14 wanachukua hatua ya kumuozesha mtoto yule kwa hivyo kesi inapokwenda wazee wanakubaliana kuwa mtoto yule ameshabakwa kwa hivyo aozeshwe. Kweli ni *solution* ya mtoto kuozeshwa mtoto wa miaka 14 hata mume hamjui. Mhe. Spika, kwa hivyo serikali nayo ielimishe jamii ielewe umuhimu wa haki ya msingi ya mtoto sio kuwa mtoto ameshabakwa halafu anaozeshwa.

Mhe. Spika, mengi yameshachangiwa na wenzangu, lakini kama mimi mwanamama nikaona kwamba kukaa kimya tu nitakuwa sijawatendea haki watoto wetu. Kwa hivyo, nichukue nafasi hii Mhe. Spika, kwa niaba ya wanawake wote wa Mkoa huu kuunga mkono hoja ya Mhe. Mgeni asilimia mia juu ya mia. Na kama kuna asilimia 200 basi naunga mkono hoja hii ya msingi ya Mhe. Mgeni, kwa asilimia 200.

Mhe. Spika, baada ya hayo basi nimshukuru sana Mhe. Mgeni Mungu ampe afya njema, Mungu ampe uzima awe na moyo huo huo na sisi tuko pamoja na yeye. Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla sijamkaribisha Mheshimiwa Kazija ningetegemea kwamba kwa uzito wa suala hili basi huu ukumbi ungekuwa umejaa, viti vyote tukaona vimejaa ili wananchi wakaelewa kwamba kwa kweli Baraza wanajadili jambo muhimu ndani ya jamii lakini hali hii haioneshi mtizamo huo.

Kwa hivyo, basi niwaombe wale Waheshimiwa walioko nje wangeingia humu tukasikilizana kile kinachozungumzwa ili hatimaye kwa pamoja tuweze kufanya uamuzi juu ya jambo hili muhimu.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hoja ya Mhe. Mgeni Hassan Juma, inayohusu udhalilishaji wa watoto. Mhe. Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa na afya na uzima tukakutana tena katika Baraza letu kupanga mambo yetu ya maendeleo ya nchi yetu.

Pili, Mhe.Spika, nimshukuru Mhe.Mgeni Hassan Juma,kwa jitihada zake na imani yake aliyokuwa nayo ndani ya moyo kuona jambo hili linafaa kutuletea sisi Wawakilishi kuweka maazimio yetu na kulichangia na kuishauri serikali yetu. Mhe. Spika, serikali ina dhamira ya kuwalinda watoto kama hivyo ndivyo niiombe serikali suala hili liwe na dhamira ya dhati kabisa kuwalinda watoto wetu, kwani watoto wetu ni taifa la kesho. Tusipowalinda watoto hivi sasa basi baadae tutakuwa hatuna taifa lililo bora na litakalotuletea tija katika nchi yetu.

Mhe. Spika, mimi naisema hii Sheria ya Mtoto ya namba 6, ya 2011 kwa namna moja au nyengine nitasema nayo inachangia kwa sababu imewapa uzito watoto kuliko mzazi. Sasa nimuombe Mhe. Waziri, aifanyie marekebisho hii sheria haraka sana ili mzazi apewe uzito kuliko mtoto wake. Mhe. Spika, mtoto huna haki ya kumpiga hivi sasa, ukimpiga ni kosa hili nalo ni tatizo linachangia. Mtoto usipomrudi tayari anakupandia kichwani.

Kwa hivyo, niiombe Wizara ifanye haraka sana ilione hili suala ifanyie marekebisho sheria hii, na sheria hii iwape uzito wazazi ili wawalee watoto wao pamoja na fursa ya kumrudi mtoto anapofanya makosa. Mtoto anafanya kosa ukimwambia hukumrudi basi yeye anazidi kupanda juu zaidi.

Mhe. Spika, kwa kuendelea mchango wangu nachangia kwa jumla ya niseme kwamba na sisi wazazi tunachangia baadhi yetu, serikali inachangia ndio kama hivyo imewapa uzito watoto na pia Jeshi letu la Polisi linachangia kwa kiasi kikubwa sana pamoja na Mahakama yetu. Kwa nini niseme hivyo Mhe. Sisi baadhi ya wazazi watoto wetu wanapofanyiwa masuala haya huwa tunakaa na kuzungumza tunasema yamekwisha. Kwa hivyo, hatuendi kulalamika kunakohusika ikafuatwa sheria, sheria ikachukua mkondo wake.

Lakini pia, na Jeshi la Polisi linachangia kwa upande wake. Mzazi ataenda kushtaki kutokana na mtoto wake vitendo alivyotendewa, lakini Jeshi la Polisi linawaita wale waliotenda suala hilo, mfano waume wanawaambia aa kwa nini hamkubaliani mkayamaliza hapa hapa kwa kuwaozesha hawa watoto.

Mhe. Spika, hili linafanyika tena sana kabisa. Kwa hivyo, niliombe Jeshi la Polisi likipelekewa taarifa kama hizi waifuate sheria inavyosema wasijifanye makungwi, wakaamua wao Mhe. Spika, hii ni hatari kubwa sana na itapelekea nchi yetu iingie ndani ya hatari. Kwa sababu watoto wetu tunawategemea baadae wapate elimu bora, wawe viongozi katika nchi hii, lakini mtoto keshatiwa mimba anapigwa mke, je, hilo taifa tutalipata tunalolitaka taifa bora wakati watoto siku zote si chini ya 70; yule katiwa mimba, yule kabakwa, tutalipata taifa hilo.

Basi niwaombe Jeshi la Polisi waache mara moja huu mtindo wao wanaoufanya wa kuamua kesi bila kuzifikisha zinakohusika.

Na nawaomba wazazi wenzangu pia wanapotokewa na matatizo kama haya waiachie sheria ifuate mkondo wake, sio kulazimishana watoto kuwaozesha, litakuwa taifa hili linarudi nyuma, tutawakosa viongozi bora, tutawakosa wataalamu, tutakosa kila kitu Mhe. Spika.

Mhe. Spika, kwa kuendelea na mchango wangu Mhe. Mgeni Hassan Juma, aliweka maazimio yake tisa na mimi nataka niseme kama ataona linafaa kulichukua kama azimio au maoni atajua yeye mwenyewe, lakini na mimi nasema. Mhe. Spika, katika azimio letu tuliweke na hili liwe kama azimio kwa kuishauri Wizara na Serikali, zinapotokea kesi niiombe hii Wizara au serikali watuwekee mawakili wanaoshughulikia kesi za watoto tu kwa kila Wilaya, kwa kila Mkoa ili kuhakikisha huyu wakili anazifuatilia kesi za watoto ipasavyo na kujua mwisho wake. La si hivyo, Mhe. Spika, maisha tutakuwa tunanung'unika na tunasema taifa linaharibika. Mhe.Waziri, nimuombe hili alifanyie kazi.

Na jengine niliombe Mhe. Spika, sisi wanawake wanapotuchukua waume, kwa kutuoa na baadae wanapoamua wao wenyewe kutupa talaka kutuacha huwa wanatutelekeza pamoja na watoto wetu. Sasa Mhe. Spika, hili nalo tatizo kubwa sana na linalopelekea watoto kuwa mfarakano hata kutopata malezi bora ya wazazi wao wote wawili.

Sasa naishauri serikali hapa napo ituwekee sheria, sheria ambayo itakayotufanya sisi wale wanaume watakapotuacha na wale watoto iwalazimishe wawe wanawashughulikia ipasavyo, wanawapatia haki zao zote zamsingi za watoto pamoja na yule mzazi.

Kwa sababu tayari ushamtwika mzigo, ukimtwika mzigo, mtoto wakati unamlea wewe mzazi wa kike, mtoto hawezi kukusikia, lakini akianza na yeye mwenyewe kumuwekea mazingira mazuri, sisi tunakuwa jukumu letu ni la kusaidiana basi. Mimi nahakikisha watoto wetu tukiwa tutawalea vizuri na wataendelea vizuri, lakini kwa kusema mzigo wanatuachia sisi wanawake tu, hali ngumu watoto watabakwa Mhe. Spika siku zote, kutokana na maisha tuliokuwanayo magumu na hilo taifa bora hatulipati.

Lazima serikali ilione hili na itufanyie haraka sana ya kwamba waume wanapotuacha lazima watusaidie watoto kutokana na maisha yetu, kwa sababu watoto wanakuwa wanasambaratika mara yuko kwa shangazi, mara leo kwa mama, hana mastakimu maalum, mtoto huyo asibakwe, anangojea nini Mhe. Spika. Basi naiomba serikali na hilo ilichukue.

Mhe. Spika, kwanza naunga mkono kwamba mtaala huu uingizwe katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kuanzia skuli ya msingi yaani chekechea ili watoto kujijua, kufahamu nini maana ya ubakaji, nini kubakwa na nini kudhoroteshwa maisha yao kwa kupatiwa mimba za utotoni. Hili naliunga mkono, lakini Mhe. Spika, kwenye hizi jela zetu watoto wanachanganyishwa pamoja, nako kule vitendo hivi vinafanyika. Mtoto akitolewa kule amebakwa, akishatoka nje amekuwa khanisi, ndio tuna taifa bora hivyo, lazima serikali na hili iliangalie kwa kina watoto jela wawekewe sehemu yao maalum ili waondokane na kadhia hii.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naiunga mkono hoja ya Mhe. Mgeni Hassan Juma, kwa asilimia mia moja.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, nami sina budi kwanza kutoa shukurani zangu za dhati kumshukuru Allah (*S.W*) kwa kutujaalia kuwa wazima wa afya na tukaja katika siku hii ya leo *Yaumul-Jumaa* kuendelea kuzungumza na hoja iliyo mbele yetu.

Lakini pili, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi yako hii adhimu na nilipoingia nilikuwa nishakata tama, kwamba una desturi ukishamwita mtu mara nyengine humwiti tena. Lakini nashukuru kwa kunifanyia ihsani hiyo kubwa na mimi nikaweza kufika hapa na kuweza kutoa maoni yangu mawili matatu niliyonayo.

Mhe. Spika, la tatu, nimshukuru Mhe. Mgeni Hassan Juma. Mimi niseme kwamba toka kuundwa kamati za Baraza na hasa hii Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, huyu mama ameonesha mfano. Huko nyuma sina kumbukumbu vizuri sijui, lakini kwa kipindi hiki cha miaka mitatu tunayokwendanayo hii kamati itakuwa ni mara ya pili.

Kwa hivyo, Mwenyekiti huyu ni mpya wa kamati hii, ameonesha mfano kwamba katika kutembelea kwenye maeneo mbali mbali hii kadhia ipo na ishaota mizizi katika nchi yetu ya Zanzibar. Kwa hivyo, amejitolea ili kuwafanya watoto wa Kizanzibari wawe ni watoto ambao wana maadili mazuri na wana heshima kama vile zamani ilivyokuwa.

Lakini Mhe. Spika, jambo lolote haliji tu hivi hivi linahitaji uangalizi na usimamizi. Kwa hivyo, jitihada aliyochukua Mhe. Mgeni Hassan Juma, kuifikisha hapa mbele ya chombo hiki hoja yake ni kubwa na mimi namuingiza katika wale wanawake majasiri na yeye ni miongoni mwa wanawake hao. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nikubaliane na wale ambao wote wamewahi kuichangia hoja hii na wakaiunga mkono. Mimi hii hoja siipi asilimia mia moja, naipa asilimia 250.

Mhe. Spika, katika hoja hii imejionesha mwenendo wa kesi za watoto zinazofikishwa katika Mahakama, ametueleza kwamba mwaka 2010 kesi 48 zimefikishwa Mahakamani, lakini mwaka 2011 kesi zile hazikupungua, bali ziliongezeka zaidi zikafika 74, maana kama kwamba waliambiwa vijana hili jambo ongezeni juhudi.

Kinachopelekea hivyo Mhe. Spika ni nini, ni hukumu ambazo hazileti mwelekeo. Sasa ikishakuwa hukumu haileti mwelekeo, watu wanapelekwa hatima yake wanaambiwa hakuna kesi, lazima watu watafanya juhudi zaidi, afadhali huu mwaka uliopita wa 2012 zimefikia kesi 72. Kwa hivyo, kule tulikuwa na kesi 74 mwaka 2011 na 2012 kesi 72.

Lakini niseme Mhe. Spika, hizi ni zile kesi tu zilizopelekwa kule, lakini zilizokuwa hazikupelekwa Mahakamani ni nyingi zaidi kuliko hizi. Kwa hivyo, ukitizama mazingira ya Zanzibar kwa hali hii tuliyofikia, miaka ya mbele tunayokwenda Zanzibar itapoteza vijana wake karibu asilimia 90.

Sasa Mhe. Spika, kama wimbi la vijana ni hivyo ambao ndio viongozi wanaotarajiwa kuja kuiongoza nchi hii kuwa marais, mawaziri na maafisa mbali mbali ikiwa hali ni hii inayoendelea hili litakujakuwa taifa gani, hilo litakujakuwa ni taifa baya sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika, mambo haya yanayotuingilia sasa ya kijuujuu mambo ya utandawazi ni hatari sana kwa Wazanzibari na huu uhuru tunaokwenda nao wazee kukosa haki ya watoto wao, basi kama hatutaamka mapema tutaendelea kuchelewa huku huku tutawakosa vijana.

Mhe. Spika, utandawazi tulionao sasa hivi dunia ni kiganja, unaweza kuiangalia dunia popote pale ulipo. Kikubwa Mhe. Spika, kinachowafanya vijana waharibike zaidi ni simu. Simu imekuwa ni tishio na kwa taarifa yako Mhe. Spika, hapa Tanzania sehemu inayoongoza kwa simu nyingi ni Zanzibar. Zanzibar imekuwa ni tishio kwa watu wenye simu, simu zipo aina mbali mbali, lakini baadhi ya mashirika mengine yanayotengeneza simu vijana wengi hawazitaki hizo, watu wamehamia kwa Mchina bwana, simu za Mchina zinaleta sura mbaya kwa nchi yetu, simu hizi za Mchina hakuna kitu kilichobakishwa hapo.

Sasa vijana wetu ndio simu wanazonunua hizo na huko kila kitu unachokihitaji utakikuta wewe. Mhe. Spika, kitu kibaya mno katika mambo basi ni kuona. Kama unavyosikia macho yakishaona yanapeleka taarifa kwenye akili na akili itachambua na kufanya maamuzi. Sasa wakati haoni kijana mmoja wala mtoto mmoja, ni watoto wengi wanaona. Kwa hivyo,

lazima na yale matendo wanayoyaona mle watasema haya si bure, kwa vyovyote kuna ladha na mvuto fulani.

Kwa hivyo, vijana wanazama hapa, sasa hili ni tatizo Mhe. Spika. Hapa Zanzibar nyumba moja kama ina watoto sita, basi amini usiamini vijana wanne wa nyumba hiyo wana simu. Kwa hivyo, tutafika wapi na simu inayochaguliwa zaidi ni Mchina.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, tukiendelea kwamba tunaheshimu sana haki za kibinadamu, lakini hizi haki hazina mpaka. Hakuna sheria isiyokuwa na mpaka, kwa sababu kijana anaweza kuamua kuiba akaona ni haki yake yeye anayoifanya, mimi haki yangu niibe, akili zake zote ndiko zinakompeleka. Sasa huyo akiiba sheria isimtie mikononi kwa sababu ndio mapenzi yake yeye kaona bwana mimi niibe.

Jana hapa Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, alizungumza kuwa kijana kuzuwiwa na wazazi wake asitizame televisheni saa sita za usiku na kuendelea, haki yake na maamuzi yake yamempa afanye hivyo. Kijana yule kufika skuli walimu wakaja wakalifuatilia tatizo lile mpaka kwao. Sasa huko ndiko wenzetu wanakotaka watupeleke kwamba wewe mzee usiwe na uzito wowote juu ya mtoto wako. Mhe. Spika, tukienda hivyo tukiwafuata watu wanavyokwenda katika nchi zao, tutafika pabaya.

Mhe. Spika, Mwenyezi Mungu ameumba ulimwengu wake aujuwae mwenyewe alivyouumba na kila sehemu kaweka watu wake ndani alivyowaweka mwenyewe. Kwa hivyo, watu wote katika ulimwengu hawalingani kifikra, kimawazo, kiakili na mambo mengine; wengine ni wapole, wengine ni majabari sana, wengine wasikivu, wengine hivi tunavyoona sasa huko duniani sehemu mbali mbali watu wamo katika vita, lakini sio kama nchi nyengine wote wataingia kwenye vita hapana, wengine kama huku kwetu tuko shuwari kabisa.

Kwa hivyo, hayo ndio maumbile ya dunia ilivyo. Sasa na sisi kuwa kwetu rahisi tukaachia uhuru maana tumeacha uhuru mpaka wa namba ya mwisho kabisa, hili ni tatizo Mhe. Spika, hiki kizazi kitakwenda na maji.

Mimi Mhe. Spika, hivi karibuni mwezi huu wa Mfunguo Nne katika jimbo langu kulifanyika maharusi mbali mbali, watu walikwenda wakachumbia mtoto baada ya kuchumbiwa wakenda kuowa. Lakini yule mume anakaribia pale kwenda kuowa mwari kaumwa na tumbo, kuumwa na tumbo kapelekwa hospitali alipofika kule kazaa mtoto wake bi harusi hata hakuwahi kufunga ndoa, kumbe tayari huku nyuma watu washafanya waliyoyafanya, maharusi

wakarudi na hudhuni na wale kule wana kilio kwamba harusi wao tayari ameshazaa kabla ya kuolewa.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, hali kama hii kwa kweli ni tatizo na ni kweli kwamba Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Baraza lililopita alileta swali hapa akasema kwamba, vijana wengi hasa visiwani Pemba baadhi ya maeneo wanaume wanabakwa. Kwa hivyo, wabakaji ni nani, wabakaji ni sisi kwa sisi, ni familia hizi hizi lakini kukosa ule moyo wa kusimamia na kuona kwamba huyu hilo analolifanya hii si haki ya binadamu kama mwanadamu huyu amdhalilishe mwanadamu mwengine si haki. Sasa hili bila ya kulisimamia Mhe. Spika, hatutofika.

Leo nimesikia kwenye vyombo vya habari jana wenzetu wa Uganda wamepitisha sheria ya mavazi, wamepitisha kabisa na wameisema wazi kwamba, mwanamke yeyote yule atakaevaa nguo nusu uchi au nguo za kubana basi mtu huyo atafikishwa Mahkamani na ikidhihirika ana miaka miwili jela. Sasa la kusikitisha sheria hizi hizi hapa Zanzibar zipo, zipo kabisa lakini mambo yote tunayaacha haya yaache yaende leo wenzetu unaona wameshafikia hatua hiyo.

Lakini leo hapa petu mila yetu haituruhusu kwenda hivyo, dini zetu hazituruhusu kwenda hivyo, lakini tumekuwa rahisi mpaka namba ya mwisho Mhe. Spika. Kwa hivyo, ningeliomba sana sisi Wawakilishi, mapolisi wanaosimamia nchi hii ili vijana wetu hawa waweze kutokufanyiwa maovu kama haya kudhalilishwa ya kulawitiwa, ya kubakwa basi ni lazima hizi sheria tuzisimamie, kama hatutosimamia hizi sheria wakati zipo na bado hazijafutwa tutakuja kila siku hapa tukipiga kelele hatima yake hakuna linalokuwa.

Mhe. Spika, nashukuru kwa kunistahamilia kote huko. Mwisho nasema kwamba mimi na watu wa Jimbo langu la Tumbe hii hoja tunaiunga mkono ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru na mimi kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Pili, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa tukiwa na afya nzuri. Lakini la tatu naomba nimshukuru Mhe. Mgeni Hassan Juma, kwa kuleta hoja yake binafsi inayohusu juu ya udhalilishaji wa watoto Zanzibar.

Mhe. Spika, Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto ina jukumu la kulinda na kutetea haki na maslahi ya watoto Zanzibar, hili ndilo jukumu kubwa tulilonalo wizara yetu.

Mhe. Spika, nataka nieleze jitihada mbali mbali ambazo zinachukuliwa na wizara yetu katika kupambana na kuondoa suala zima la udhalilishaji ambalo lipo Zanzibar. Katika kuhakikisha jukumu hili linafikiwa Mhe. Spika, Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto imeandaa yafuatayo katika kupiga vita udhalilishaji wa watoto.

Kwanza, imeandaa sheria ya mtoto, Sheria Nam. 6 ya mwaka 2011 ambayo sheria hii Mhe. Spika, hukumu za kubaka zimeelezwa katika sheria na kama uthibiti ukitokea basi aliyefanya kosa anatakiwa ahukumiwe miaka…

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kuna mkutano mwengine pale, tungeomba tumsikilize Mhe. Waziri anachangia kwa madhumuni ya kuifanya hoja hii iwe bora zaidi. Mheshimiwa endelea.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Hukumu zinaonesha katika sheria na sheria ipo na inafanya kazi na kanuni tayari tumeshaziandaa. Hukumu iko wazi kwamba mbakaji wa watoto wadogo hata mtu mzima ikithibitika afungwe kifungo cha miaka 30. Sasa sijui kwa nini watu wanapata wasi wasi wa kuona kwamba kama sheria hii haifanyi kazi. Sheria inafanya kazi vizuri sana lakini bado haijapewa nafasi ya kufanya kazi.

Sasa hivi Mhe. Spika, tunajiandaa na kufanya sera ya uhai, hifadhi na maendeleo ya mtoto na karibu itakuwa tayari sera hiyo. Nia ni ile ile ya kumhifadhi huyu mtoto.

Mhe. Spika, sisi tumeandaa kamati maalum ya Makatibu Wakuu, Maafisa wa ngazi za juu kwa ajili ya kusimamia shuguli hii ya watoto ambayo kwa kweli inatutia katika suala la aibu kubwa. Viongozi mbali mbali wanahusika, Viongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali; Viongozi wa Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, Viongozi wa Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma; Wizara ya Afya; Kamishna wa Polisi; Mkurugenzi wa Mashtaka; Mrajis wa Mahkama Kuu; *Save the Children*; *UNICEF*. Wote hawa tunakaa pamoja kwa ajili ya kuboresha uratibu wa shughuli za hifadhi na ulinzi wa watoto kwa ngazi ya juu.

Mhe. Spika, kama hiyo haitoshi tumeandaa kamati za hifadhi ya mtoto ya kitaifa na kiwilaya za watendaji zinazojumuisha wajumbe kutoka taasisi za serikali na zisizo za kiserikali. Zote hizi zinafanya kazi ya kuimarisha mfumo wa ulinzi wa watoto kwa kufanya kazi kwa mashirikiano pamoja na ufuatiliaji wa kesi na taarifa mbali mbali za udhalilishaji wa watoto.

Mhe. Spika, Wajumbe hao wanatoka katika taasisi mbali mbali ikiwemo Wizara ya Afya, Wizara Elimu na Mafunzo ya Amali; Wizara ya Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma, Chuo cha Mafunzo, Polisi, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, *ZAFELA,* Kituo cha Huduma za Sheria, Maafisa wa Ustawi wa Jamii Wilaya, Jumuiya za Wazazi ya Watoto wenye Ulemavu wa Akili na Jumuiya za Watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI.

Mhe. Spika, tumechukua nafasi ya kuanzisha vituo vya *One Stop Centre* na sasa hivi vimeenea mijini na vijijini, Pemba na Unguja kwa ajili ya kufanya kwamba mtoto anapobakwa ushahidi usipotee pale pale, anapelekwa katika kituo hiki cha mkono kwa mkono na pale watu mbali mbali wapo wanaohusika na ushauri nasaha, ushauri wa kisheria na kadhalika. Lakini bado kabisa hatujafanikiwa vizuri.

Mhe. Spika, tumeanzisha na kuzinduliwa kwa Mfumo wa Kitaifa wa Kuhifadhi taarifa za udhalilishaji yaani *(Child Protection Database Management)* ambapo taarifa za matokeo yote zinahifadhiwa pale na zinakuwa zipo zinajulikana na zinafanyiwa kazi.

Mhe. Spika, tunashirikiana na Dawati la Jinsia na Watoto katika kutetea haki na ustawi wa mtoto. Tumeanzisha Kamati za Jinsia na Watoto katika ngazi za kitaifa na wilaya, zote hizi zinajumuisha Wajumbe kutoka katika serikali, Taasisi za Dini, Wawakilishi, Masheha, Mwakilishi wa Vijana, Mwalimu wa Skuli, Polisi, wote tunawashirikisha ili vitendo hivi angalau vionekane kwa urahisi na vifanyiwe kazi.

Wizara yetu hii ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jami, Vijana, Wanawake na Watoto tukishirikiana na *Save the Children* na *UNICEF* tunatayarisha machapisho mbali mbali ambayo kwa namna moja au nyengine yanasaidia katika kutoa taaluma kuhusu majukumu ya Kitengo cha Hifadhi ya Mtoto.

Machapisho hayo ni miongozo ya kitaifa ya hifadhi ya ustawi wa watoto Zanzibar, miongozo hiyo inatoa taarifa mbali mbali kama, Muongozo wa Utekelezaji wa Kulinda na Kuhifadhi Watoto Zanzibar, Daftari la kukusanya taarifa ya udhalilishaji na kadhalika. Daftari limekusanya fomu ya utoaji wa taarifa za udhalilishaji wa mtoto katika ngazi ya shehia ambalo hujazwa na waratibu wanawake na watoto kwa kushirikiana na masheha katika ngazi ya shehia. Zote hizo ni jitihada za serikali kwamba kwa vyovyote pale likitokea tatizo kuhusu kudhalilishwa kwa mtoto basi hatua zianze kuchukuliwa.

Tumetengeneza muongozo wa uanzishwaji wa nyumba za kulelea watoto Zanzibar, tumetengeneza kitini cha kitaifa cha hifadhi ya mtoto Zanzibar, muongozo wa taarifa za huduma za watoto ambapo taarifa za mawasiliano na

wadau na watendaji mbali mbali zimeainishwa na kugawiwa kwa masheha na taasisi nyengine kurahisisha mawasiliano.

Mhe. Spika, hapa watu walikuwa wanasema kwamba vitendo vinavyofanywa ni vitendo vya kinyama kwa watoto wadogo. Lakini nisema Mhe. Spika, kwamba si vya kinyama ni vitendo vibaya, kwa sababu mnyama Mhe. Spika, hawezi kuzini, hawezi kubaka, hawezi kulawiti, anafanya mambo yake kwa utaratibu kama alivyowekewa na Mwenyezi Mungu, lakini sisi tunafanya vitendo vya kikatili sana kwa watoto wetu.

Mhe. Spika, mimi nataka niseme kwamba namuunga mkono sana Mhe. Mgeni Hassan Juma na kwa bahati nzuri huyu ni Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii. Kwa hivyo, *inshaallah* tutakuwa pamoja na tulikubaliana kwamba hili jambo analolileta hapa sio lake peke yake lakini ni la wanawake sote tuliomo katika Baraza hili.

Mhe. Spika, kulikuwa na tatizo moja lililozungumzwa kwamba watoto wanachanganywa na watu wazima kwenye Chuo cha Mafunzo. Suala hili Mhe. Spika, tumelishughulikia na sasa hivi watoto wako mbali kabisa na watu wazima hawachanganywi kwa pamoja.

Mhe. Spika, naomba niseme kwamba mimi naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na nampongeza tena Mhe. Mgeni Hassan Juma, kwa kuleta hoja hii. Mimi niko pamoja naye damdam na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatufikisha pahala pazuri. Ahsante kwa hilo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, kwanza na mimi naomba kuchukua fursa hii baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya na uwezo wa kuweza kufika na kuchangia katika hoja hii muhimu, kukushukuru na wewe mwenyewe binafsi kwa kunipa fursa hii.

Lakini la pili, na mimi naomba niungane na wenzangu kumpongeza sana Mhe. Mgeni Hassan Juma kwa kuandaa hoja hii, kwanza kwa kufikiri, kwa kuguswa na tatizo hili na kuandaa hoja hiyo. Mhe. Spika, hiki ni kielelezo kwamba Mhe. Mgeni Hassan Juma, sio tu anang'ara kwa sura yake, lakini pia anang'ara katika moyo wake. *(Makofi/Vicheko)*

Na bila hayo ninaamini asingeweza kuandaa, kuguswa na jambo hili kwa kiasi alichoguswa na kuweza kuandaa hoja hii. Kwa hivyo, tumpongeze sana kuliko tunavyopongeza.

Lakini la pili, na mimi niungane na wenzangu kusema kwamba hili tatizo ni kubwa kuliko wengi tunavyolifikiria kusema kweli na ukubwa wa tatizo hili

ni kwa sababu tu zile kesi nyingi zinazotokea haziripotiwi katika vyombo vya habari, haziripotiwi katika vyombo vya kusimamia sheria.

Lakini athari yake kusema kweli Mhe. Spika, ni kubwa sana. Mhe. Amina Iddi Mabrouk, alizizingumza hapa ile athari ya vitendo hivi kwa watoto. Na moja katika athari yake kubwa ni kile ambacho yeye amekieleza vizuri sana, ile wanaita kwa kizungu *trauma*, kwamba inamkosesha mtoto ile *confidence* ya uwezo wake wa kukua akili yake ikiwa huru kwa muda wake kwa maisha yake yote kusema kweli. Kama kuna kitu ambacho kinamjeruhi na kumuachia kovu katika maisha yake yote basi ni vitendo hivi vya kudhalilishwa wanavyofanyiwa watoto.

Na ukitaka kujua hili kuna wenzetu ambao wamelifanyia kazi hili na wameigiza michezo mingi kusema kweli, kuonesha kwamba mtoto kufanyiwa kitendo cha namna hii basi kinamuathiri katika maisha yake yote. Wengine wameonesha jinsi gani mtoto anakuwa na yeye mwenyewe anakuwa na tabia ya chuki, anakuwa na tabia ya kuchukia baadhi ya watu na anakuwa na vitendo vya ajabu katika maisha yake yote.

Unaweza kumkuta mtu mwepesi wa kukasirika, unaweza kumkuta mtu mwepesi wa kupigana na watu kumbe ni matokeo ya vitendo hivi ambavyo alifanyiwa akiwa mdogo na bahati mbaya vikawa havikupata tahafifu, yaani hakutendewa haki katika kurekebishwa lile ambalo lilitokea dhidi yake.

Tutalizungumza sana Mhe. Spika, lakini kiini cha tatizo hili, mimi ninadhani ndio muhimu tukizungumza. Katika mfano mwengine Mheshimiwa mmoja alisema kwamba tusizungumze tulipoanguka, mimi ninadhani ni muhimu sana katika jambo kama hili tuzungumze zaidi tulipojikwaa.

Mhe. Spika, kwa kweli kiini cha tatizo hili ni mambo mengi sana kusema kweli. Tunaweza tukakaa tukawalaumu watu wasimamizi wa sheria, ni kweli wana mchango mkubwa, tunaweza tukawalaumu wanaofanya upepelezi ni kweli wana mchango mkubwa, tunaweza tukawalaumu wazazi na ni kweli wana mchango mkubwa.

Lakini huo mchango wao kwa ujumla yao, kwa nini mtu kapewa kazi ya kusimamia sheria na haguswi na tatizo hili Mhe. Spika, ni kwa sababu ya kuporomoka yale maadili ya kijamii, ni kwa sababu ya kuporomoka silka tulizokuwa nazo. Na hizi ndio hata dini yetu inavyotufundisha kwamba yakiondoka haya, basi mengi yatakuja kusema kweli. Maana kama kuna jambo ambalo tunasema ni ufisadi na linalostahiki kuitwa hivyo, basi ni jambo kama hili.

Sasa ni bahati mbaya kwamba haya yameporomoka katika kila upande. Kwa hivyo, mimi ninaomba sana wenzangu tuliangalie hili jambo kwa upana wake na tutafute kiini cha tatizo. Lakini sehemu kubwa, hili tatizo tukiliangalia sheria tunaweza tukasema na usimamizi wa sheria ni asilimia 30, lakini asilimia 70 kwa kweli ni suala la kijamii.

Na ninasema hivyo kwa sababu si nia ya kuvunja moyo au kusema kwamba aah! usimamizi wa sheria hauhitaji kuwa madhubuti, unahitajika kuwa madhubuti sana. Lakini kama kuna kitu ambacho kinahitajika kuwa madhubuti sana ni utamaduni wetu, mila zetu, silka zetu na maadili yetu kwa ujumla.

Kuna mambo tunaacha tunafikiria athari yake ni ndogo lakini kusema kweli athari yake inatufikisha hapa tulipofika hii leo. Dini yetu kwa mfano imetufundisha akinamama wazibe vichwa vyao, mwengine anaweza akaona ni jambo dogo kwa sababu yeye hapendi nywele, lakini mwengine ndio wazimu wake. Kwa hivyo, hiyo ni sehemu ya kinga na huwezi kumjua, nani mwenye wazimu wa nywele na nani hana wazimu wa nywele. (*Makofi*).

Kwa hivyo, imewekwa ile kinga mapema na ukisema wewe unaidharau basi athari yake inakuja. Walipoambiwa shungi ziteremke mpaka kifuani, aliyetunga sheria hii anajua kwamba wengine wazimu wao ndio humo. Kwa hivyo, ukidharau wewe unaweza ukaona ni jambo dogo lakini kusema kweli unakusanya zile athari kwa athari mpaka unafika pahala unakuwa tatizo kubwa katika jamii. (*Makofi*).

Sasa na haya mambo kuna mengi tumeyaacha vile vile na moja tulililoliacha kusema kweli sasa kuna mambo mengi, tulichukulie mtu yeyote sasa hivi mtoto na mtu mzima ukiangalia gazeti maana yake kuna uchochezi. Maana uchochezi tukiita zamani tu kwenye siasa lakini sasa hivi kumeingia uchochezi wa namna hii. Kwenye magazeti, ukisikiliza nyimbo takriban asilimia kubwa za taarab na kila aina zote ni za uchochezi. Ukisoma gazeti ni uchochezi, sasa unajiuliza huyu unayemchochea baadae ndio aende pahala gani. Ndio matokeo yake tunajenga maradhi ya akili kwa sababu wataalamu wa masuala kijinai wanasema kwamba unapoona tatizo la namna hii, yaani tabia au hulka ya ajabu ajabu ya namna hii, kwa sababu hii ni hulka ya ajabu.

Mhe. Zainab Omar Mohammed, pale amesema kwamba aah! wanyama hawafanyi hivi na mimi ninamtetea, kusema kweli mtu kusema hivi ni vitendo vya kinyama ni kuwaonea wanyama. Maana yake wanyama hawafanyi vitendo vya namna, hii zaidi ya vitendo vya kinyama, sijui tuviite vya namna gani. (*Makofi*).

Sasa ukiviona vya namna hii ni kwamba muna tatizo, ama kuna ugonjwa umeingia ama muna matatizo ya kimazingira, unasema *circumstances*, hivyo munavyoishi kuna tatizo munalisababisha mpaka mumefika hapa. Sasa mimi ninaamini kwamba huu ni ugonjwa kwa sehemu moja lakini pia ninaamini kwamba tuna tatizo katika tunavyoendesha maisha yetu mpaka tumefika hapa. Na tumefika hapa Mhe.Spika, kwa sababu imeanza kuondoka watu kuchukia vitendo vya namna kama hii. Kwa sababu gani, haya mengi yaliyozungumzwa hapa mimi nimekaa kwenye taasisi hizi kwa muda mrefu kusema kweli. Na unashangaa na haya alisema hapa Mhe. Salmin Awadh Salmin baba mtu kamuingilia mtoto, mama mtu ndio hataki kuja kutoa ushahidi, anamlinda baba mtu na ushahidi upo wazi.

Hivi viteno vya kusema kwamba kupata ushahidi katika nini, tunawalaumu Mahakimu ni kweli wapo ambao hawaguswi na haya, rushwa pia imo katika hili. Mimi ninasema ukifika pahala ikiwa mtu anachukua rushwa kwenye jambo la namna hii, kusema kweli hapo una tatizo kubwa sana. Ndio ile tunarudi kule kule kwamba kuna tatizo katika tunavyoishi kwenye jamii mpaka tumeweza kufika hapa, ubinadamu kwamba umeondoka.

Kwa hivyo, ninasema haya kwa sababu ni muhimu sana katika hili tusizungumze tu, ni muhimu sana kupata lile suluhisho tukalipatia vizuri. Mimi ninasema kwamba katika maazimio ambayo Mheshimiwa mtoa hoja Mhe. Mgeni Hassan Juma, ameyatoa kusema kweli yote ni ya msingi. Moja katika la msingi kusema kweli ndio pale aliposema kuandaa mkakati wa kitaifa, kwa sababu tutakapoandaa mkakati wa kitaifa ninaamini kwamba pale mambo mengi tutapata kuyaangalia kwa upana wake, yale mengine yote yaliyopendekezwa basi yatamezwa na lile moja la mkakati wa kitaifa.

Kwa hivyo, mimi naona lile ni la msingi sana na mengi tumependekeza Mhe. Spika, mimi ninaomba sana kwamba tutafute kiini cha tatizo na kwa dhati kabisa tukitafutie dawa kiini cha tatizo. Sheria itatusaidia, lakini kusema si suluhisho. Kwenye sheria kuna ujanja mwingi wa halali na wa haramu. Tukisema tuwahasi sijui utamuhasi pahala gani. Maana anayetaka kuharibu si lazima atumie hapo utakapomuhasi, atatumia kwengine na tatizo lake si huko utakomuhasi, tatizo lake lipo hapa, lipo kichwani.

Mimi kusema kweli ni jambo ambalo naomba tulizungumze kwa dhati na hili ambalo amelizungumza Mhe. Mgeni kwamba kuwe na mkakati wa kitaifa. Hili kusema kweli ndio jambo muhimu sana sana. Haya mengine yataingia, maana yake haya mengine ninadhani yana *support*, lakini jambo la msingi, hili jambo ni lazima tukae chini tulifikirie na tuliandae mbinu za kuweza kupambana na hili tatizo lenyewe.

Mimi hapa naomba sikukusudia kusema sana, lakini naomba niseme moja ambalo ninadhani tumeliacha au tumesahau. Nalo ni hili, maana yake maazimio mengi haya tumeyaelekeza kwa serikali zaidi. Mhe. Spika, hili serikali itafanya, lakini kwa sehemu ndogo sana. Mimi ninaliona hili ndio jambo hasa la Wawakilishi wenyewe.

Humu sisi wenyewe Wawakilishi hatukujipa *role*, sisi kama Wawakilishi tumeunda jumuiya; kuna jumuiya za kupambana na ukimwi, tuna jumuiya gani tunafanya mambo mengi. Lakini kama tuna pahala pa kuunda jumuiya humu ndani ya Baraza la Wawakilishi, basi ilikuwa ni ya kupambana na vitendo vya namna hii.

Mhe. Spika, kama kuna pahala ambapo kwa dhati kabisa ninasema pa kuandaa mkakati wa pamoja humu ndani ya Baraza na ukasimamiwa, Pia, humu ndani ya Baraza, kwa sababu sisi ndio tunaokaa na wananchi. Tunayasikia haya yote, mimi huwa ninawaambiwa wenzangu siku zote mpaka ukamuona mtu kaja ofisini, kakushtakia pale Afisi ya *DPP* au kwa Mwanasheria Mkuu au kwa Mrajis wa Mahakama, ujue huyo kashahangaika kweli kweli mpaka kafika pale.

Sasa Waheshimiwa Wawakilishi haya tunayapata sisi *first and information*. Na kama tunapata *first and information* sisi ndio tutakuwa wasimamizi wazuri wa suala hili. Kwa hivyo, mimi nilikuwa naomba katika maazimio ni kwamba Baraza lenyewe liunde chombo, liunde mkakati, liunde utaratibu wa kuweza kushiriki kikamilifu katika kupambana na tatizo hili. Tukifunga mikono tukasema tunaiachia serikali tuje tuiulize, itajibu.

Lakini majibu ya serikali si suluhisho. Itakuja itatwambia pesa kidogo. Mhe.Bi. Zainab atakuja atasema mimi nilihitaji milioni thamanini, nimepewa milioni mbili, nitafanyia nini.(*Makofi*).

Sasa tutarudi kule kule kwa ile hadithi ya watengenezaji barabara. Maana kuna watu walikuwa na barabara yao mbovu, asubuhi walipoamka wakajua wakaona watu wamekuja na magari na nini, wakajua leo barabara itatengenezwa. Lakini waliporudi jioni wakakuta kumbe kumebandikwa kibao tu barabara mbovu endesha pole pole. (Makofi).

Sasa na sisi kwa utaratibu huu Mhe. Spika, na kile kibao wakaking'oa wakasema na sisi tunajua haja barabara yetu itengenezwe. Sasa na sisi ninaogopa kwa utaratibu huu tunaweza tukaja tukabandika kibao, tuna tatizo, watoto wanadhalilishwa. Watu watakuja kuking'oa kibao hicho.

Kwa hivyo, naomba sana tena kwa dhati kwa sababu na mimi ni mzazi ni mlezi, msimamizi wa sheria, naomba kwa dhati kabisa kwamba Wawakilishi katika hili tushiriki kikamilifu kama Wawakilishi na kuwashirikisha na wenzetu huko chini Madiwani, Masheha na wengine katika hili na tulisimamie. Ninaamini kwamba hilo litasaidia zaidi, litakuwa na nguvu zaidi tukichanganya na haya ambayo yanapendekezwa katika hii hoja, tutaweza kuwa na kitu kizuri cha kusimamia.

Kwa hivyo. Mhe. Spika, mimi nilisema mchango wangu ni mdogo uwe ni huo na niseme kwamba na mimi ninaunga mkono hoja iliyotolewa na fikra hii iliyotolewa na ninaahidi kushirikiana na kila taasisi ambayo itakuwa dhati kabisa itakuwa na nia ya kuweza kusimamia jambo hili ili kuliondoa hili tatizo.

Ninakushukuru sana Mhe. Spika. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, na mimi ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii lakini pia naomba nimshukuru Mhe. Mgeni Hassani Juma, kwa kuleta hoja yake hii.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa na mambo mengi kidogo sana na pengine nitakuomba kama sikumaliza nipate japo dakika 10 jioni. Hii ni kwa sababu kuna mambo ambayo ni ya jumla na ya si kitaifa lakini ni kimataifa.

Hoja hii au matatizo haya yalizungumzwa sana katika Jumuiya ya Afrika na Jumuiya ya Afrika ikatoa agizo kwa serikali za nchi zao kwamba lazima lipatiwe ufumbuzi. Sasa baada ya kutoa agizo hilo, mikutano mingi ilifanywa na mkutano mkubwa ambao ulijumuisha takriban mawaziri wengi wa Afrika wanaohusiana na mambo ya jinsia pamoja na mawaziri wanaohusiana na sheria ulifanyika Zaire mwaka jana.

Sasa huu mkutano wa Zaire ulikuwa na mambo mengi na ulikuwa na maazimio ambayo maazimio yaliyotolewa kidogo yanakwenda si kinyume, lakini yanapingana na maazimio ambayo Mhe. Mgeni Hassan Juma ameyatoa. Kwa hivyo, mimi mwisho nitaomba nirekebishe au nitoe yale maazimio ambayo ninahisi kwamba yanakwenda sambamba na hiyo taarifa ya mkutano huo wa Zaire.

Lakini la pili, Mhe. Spika, ninapenda niseme kwamba sisi tumeyapata matatizo haya kama alivyosema Mhe. Bi. Zainab, lakini naomba tutizame Waheshimiwa Wawakilishi ni nini hasa matatizo ambayo tunayo katika kulitekeleza suala hili. Mimi ninahisi Mhe. Spika, ni mambo manne:-

1. Kuna Polisi wana mchango wao mkubwa,

2. Mahakama wana mchango wake mkubwa,
3. Wazee wana mchango wao mkubwa,
4. Sisi viongozi tuna mchango wetu mkubwa.

Sehemu hizi nne zikiwa kweli zinataka kuyaondoa matatizo haya ninaamini tunaweza tukafanikiwa kwa asilimia kubwa sana.

Mhe. Spika, katika mkutano huo niliouzungumza wa Zaire walikuwa wanazungumzia suala la wanaita *Sexual Gender Baser Violence (SGBV)*. Na hapa waliona kwamba matatizo haya yapo si Zanzibar tu wala si Tanzania, lakini takriban nchi zote za Afrika na kwengineko, lakini wao walikuwa wanazungumzia Afrika.

Kwa hivyo, katika mkutano ule walikuwa na mambo mawili makubwa ya kuzingatia. Kwanza walisema kwamba ili kuyapunguza matatizo haya labda ama kuwe na Mahakama maalum ambazo zinazowahusisha watu hawa, yaani ziundwe Mahakama *special* kwa kuzungumzia au kwa kushughulikia kesi namna hii. lakini pia wakasema kwamba serikali ziwe zinatoa ripoti kila mwaka katika vyombo vinavyohusika vya jumuiya hiyo.

Lakini azimio kubwa lililotokea Mhe. Spika, ni azimio la kuwa na *zero tolerance* katika masuala haya. Yaani ule uvumilivu uwe haupo kabisa, tusiwe tena na kuvumilia kesi yoyote ambayo itatokea juu ya masuala haya. Na walitoa baadhi ya mambo ambayo hayo nitaomba baadae mwisho niweke kama ni maazimio kuyaongezea haya au kupunguza haya aliyotoa Mhe. Mgeni Hassan Juma, ili suala letu liwe zuri na liwe kwa mujibu wa utaratibu wa Umoja wa Afrika.

Mhe. Spika, kwa nini nikasema kwamba Polisi wana jukumu kubwa. Mhe. Spika, Polisi hawatusaidii kwa sababu tumekuwepo katika shughuli hizi kwa kipindi kidogo. Lakini Polisi wana mambo mawili muhimu. Wao wanafanya kama kwamba ndio Mahakama na wanajaribu kuwatisha baadhi ya watu. Inapotekea kesi ikapelekwa Polisi kuripotiwa, Polisi ataita pande zote mbili kutaka suala lile lisuluhishwe. Hiyo sio kazi yake.

Lakini kama upande mmoja haukataka ama Polisi ataharibu makusudi kwa sababu yeye ndiye anayechunguza au atawatisha wale, kuwaambia kwamba mutafungwa miaka ishirini, miaka mingapi, wewe baada ya kufanya suala tukawezena hapa na nini, wewe unakwenda huko. Kwa hivyo, Polisi wanaingia katika suala ambalo sio lao. Na ikiwa Polisi tutawaachia katika masuala hayo.Kwa hivyo, wanavyokwenda hatutofanikiwa.

Kwa hivyo, kuna suala zima la Polisi kwamba kuwaondoa katika suala hili kwamba hawahusiki kwa sababu wao wanafanya kituu ambacho si chao. Na hiyo Mhe. Spika, ushahidi upo wa kesi chungu nzima. Kesi inakwenda wanapeana wale, halafu wanawaita wanawatisha, halafu mtu anakuja kushitaki kwetu. Ukiwaita Polisi mwisho watafanya mambo ya uchunguzi ambao ule uchunguzi wenyewe unaonesha kwamba huu ni kupikwa na huu unamuondoa yule anayekuja kushitaki kuonekana kama kwamba hana kesi na niniMimi ninafikiri hilo kama tukiliendeleza hilo hatutofanikiwa. Kwa hivyo, moja ya tatizo ni Polisi. (*Makofi*).

Mhe. Spika, ninakubali kwamba na Mahakama zetu zina matatizo. Baadhi ya Mahakimu wana matatizo, hawaoni umuhimu wa kesi kama hizi, wanashawishiwa na wanashawishika. Kama kama alivyozungumza kuna mheshimiwa mmoja alizungumza pale ni kweli kesi kama ile utatoa faini shilingi laki tano, huyu Hakimu tunaweza tukamuuliza au tukajiuliza, tena Hakimu wenyewe ni mwanamke. Kwa hivyo, ni kwamba ni kama anashadidia suala hilo.

Kwa hivyo, ina maana baadhi ya Mahakimu wetu Mhe. Spika, ni kweli tumejaribu kuzungumza nao na tunazungumza nao, lakini wanashawishiwa kwa vishawishi vidogo vidogo vilivyokuwa havina maana. Hii ni kujivunjia tu utu wao na heshima zao kama ni Mahakimu.

Lakini la tatu, Mhe. Spika, ni wazee. Wazee wana mchango mkubwa sana na wazee ndio hasi wanaoharibu kesi hii kwa ushahidi. Kwa sababu wazee wakishakufanya watoto wao mambo hayo, hasa wale wazee ambao mtoto wa kiume na mtoto wa kike damu imegusana kidogo ni ndugu ndugu, watakuja kesi imekuwa nzuri na nini, aah! mheshimiwa basi tuachie maana yake hii tutaimaliza sisi wenyewe, tutaozana tu na nini, sisi tunaogopa kijijini pale hatuna uso na nini. Sasa hamna uso vipi, sasa kwa nini mukafanya hivyo.
Hata ukilazimisha wazee hawaji Mahakamani kutoa ushahidi. Kwa hivyo, kesi zinakufanya hivi hivi. Kwa hivyo, wazee hawataki suala hili. Hivyo, ni lazima Mhe. Spika, katika maazimio haya ya Mhe. Mgeni tutizame ni lazima kuwe na azimio maalum kuhusu wazee. Wazee ndio wanaokorofisha katika kesi hizi.

Na sehemu nyengine Mhe. Spika, ni viongozi. Mimi binafsi nimeshapata simu chungu nzima. Nitoe mfano tu lakini mfano huo sio kwamba ni yeye aliyefanya hivyo. Kwa mfano pale rafiki yangu pale Mhe. Hamza Hassan Juma, ana mtoto wake, sasa mtoto wake kwa bahati kafanya hayo mambo. Sasa Mhe. Hamza Hassan Juma, atakachofanya atanipigia simu mimi, mimi ananijua jina langu ninaitwa Abubakary Khamis Bakar, anajua cheo changu kwa hivi sasa ni Waziri wa Katiba na Sheria, lakini yote havitumii hivyo,

akipiga simu atasema rafiki yangu kuna matatizo bwana! huyu mwanao, sasa maana yake mwanawe yeye ndio mwanangu, huyu mwanao kafanya matatizo haya na yale, kwa hivyo tufanye hivi, wameshakuja watu namna hiyo.

Sio Mhe. Hamza Hassan Juma, Jibu Mhe. Spika, mimi kuna wawili niliwaambiwa kesho kutwa tuna Baraza la Wawakilishi na hilo Baraza la Wawakilishi kuna sheria ya kukinga wazee viongozi watoto wao waendelee na shughuli hizi. Basi ninafikiri huwa ameshanijua, haulizi tena. Sasa na viongozi kama tutasisitiza hizi simu kupigiana kwamba mwanangu kafanya hivi, basi hiyo kesi bwana ifanye hivyo, hatutokwenda hata kidogo.Kwa hivyo, Mhe. Spika, mambo manne haya kwa kweli yanatuumiza katika kutekeleza jukumu hili. Polisi, Mahakama, wazee na viongozi.Kwa hivyo, lazima katika maazimio haya tuwatizame watu hao au ma-*group* hayo ili sisi tuweze kwenda vizuri na azimio hili.

Mhe. Spika, kwa maana hiyo basi katika sheria zetu za jinai ni nzuri tu. Kuna makosa chungu nzima ambayo yanaanzia miaka saba mpaka miaka thalathini ambacho ni kifungo kikubwa. Faini hamna, sasa kama Hakimu atamtoza faini badala ya kumfunga miaka 25 au miaka 20, siku zote tutakuwa hatufaulu.

Na hii Mhe. Spika, nayo inongezea katika suala wazee wetu Masheikh. Kuna kesi za Masheikh akifanya kitu kidogo bas Masheik huyu ndio Sheikh yetu lakini kapitikiwa tu, unajua Mwenyezi Mungu anasema hivi. Sasa Mungu anasema hivi Masheikh lakini huyu kafanya hivi, tutazameni. Kwa hivyo, haya Mhe. Spika, ndio matatizo makubwa katika masuala haya. Na tukiweza kuya-*contain* matatizo haya mimi ninaamini tatizo kubwa la suala hili litapunguka.

Kwa hivyo Mhe.Spika, katika mkutano huo wa Zaire mambo mawili yalielekezwa. Kwanza kuwa na Mahakama zinazojadili haya, lakini sisi tuliporejea na tukaripoti hata serikalini na tukatoa ushauri wetu na ushauri huo ukakubalika. Kuwa na Mahakama ambazo tumezianzisha makusudi kwa suala hili itakuwa kidogo ni zito kwa suala letu, kwa sababu hatuwezi kuwa na Mahakama, tukateuwa Mahakimu ikawa wao wanasubiri kesi hizo. Tukasema sisi tunapendekeza tuwe na kitu kinachoitwa *Session Cases*.

Session Cases ni kesi ambazo zikitokea unamu-*sign* Hakimu kwamba unasikiliza kesi hii mpaka imalizike hakuna holidays, na hivyo ndivyo tulivyokubaliana na Mhe. Spika, hivi sasa tumo kwenye *process* ya kuzifanya hivyo, kwamba kesi zote za aina hii zitakwenda katika *Session Cases* ambazo Hakimu tutamwambia kesi hii isikilize mpaka uimalize. Hakuna kuiahirisha kwamba ninaahirisha mpaka Julai, ninaahirisha mpaka Oktoba.

Kwa hivyo zile kesi zote usikilizaji wake utakuwa kwa kipindi kifupi. Hiyo ni moja. Lakini ya pili iliyokubalika kule Zaire ni suala la vyombo vya habari, vyombo vya habari vilitakiwa kwamba kila chomb cha habari cha serikali na vilivyokuwa si vya serikali viliomo katika nchi ile, kwa sababu vile lazima vitasikiliza amri za serikali, viwe vina kipindi maalum vya kupiga vita masuala haya. Sasa vyombo hivyo ...

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nikushukuruni, hapana shaka Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria ana mambo yaliyobaki muhimu ili ayazungumze. Kwa hivyo tutegemee kwamba jioni tutamaliza na yeye na baada ya hapo nina ombi moja la Mhe. Naibu Waziri wa Afya naye ameomba kwamba ana shughuli fulani, kwa hivyo jioni naye atachangia. Baada ya hapo tumuombe mheshimiwa mtoa hoja aweze kufanya majumuisho.

Niakhirishe kikao hiki basi hadi saa 11.00 jioni leo.

(Saa 6.00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano ya hoja hiyo yanaendelea. Tulikubaliana pale mchana kwamba Mhe. Abubakar Khamis Bakary, Waziri wa Katiba na Sheria, aanze na baadae tuendelee na waheshimiwa wengine. Naomba basi nimkaribishe.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya mwanzo jioni hii, ili nimalizie pale ambapo nimepaacha. Mhe. Spika, sitokuwa na mengi sana isipokuwa ni kumalizia mambo mawili au matatu tu.

Jambo la kwanza Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo ni kwamba matatizo ya mambo ya kubaka yako hasa katika sehemu nne na nilizitaja. Lakini napenda Mhe. Spika, katika sehemu hizo nne nitowe mifano miwili ambapo nayo tuchukulie kama ni ushahidi tosha.

Kesi ya mwanzo ambayo ipo, ni kwamba mzee alimbaka mtoto wake na baada ya kumbaka mambo yote yakashughulikiwa na ushahidi ukawepo, lakini bahati mbaya sana Mhe. Spika, polisi kwa sababu ya uhusiano tu walionao baina ya mbakaji na polisi wakasema baada ya *DPP* kuidhinisha

kwamba apelekwe mahakamani, wakasema kwamba kuna ushahidi ambao unastahiki au unafanya kwamba huyu baba mtu asipelekwe mahakamani.

Ushahidi wenyewe ni upi, akasema kwamba yule mtoto aliyebakwa yaani mwanawe alikubali kuombwa radhi na baba yake aliyembaka kuwa amefanya kosa hilo na halitotokea tena, anaomba radhi na kampa pesa kidogo. Sasa hapa kutoa kesi hii ni kwamba hawa polisi wanajua matatizo kama hayo na halafu hiyo wewe mwenyewe Mhe. Spika, unajua kuwa ni *collaboration.*

Kwa hivyo, baada ya wao kuichukua kupeleka mahakamani kuwa huu ndio ushahidi zaidi kwamba yeye mwenyewe kaomba radhi kwa mtoto wake, wanasema ni ushahidi wa kusema kwamba asipelekwe mahakanani.

Kwa hivyo, ndio nikasema chombo cha polisi kinaharibu sana katika masuala hayo. Hawa mama zetu ambao wanasema, ndio wa mbele wanaosema kwamba kuna ubakaji. Lakini pia wao ndio wa mbele wanaojifanya wanahuruma sana, kwa hivyo hilo halitokwenda. Kwa sababu huyo huyo mama mtu akaja akasema basi tunaomba kesi hii mambo yamekwishapita tena na tumeshasuluhishana ni hao hao mama zetu. Kwa hivyo, mimi nafikiri hayo ni lazima tuwe *serious,* tukiwa *serious* nayo basi suala hili litakwenda kama tulivyolipanga.

Mhe. Spika, kama nilivyosema ni kwamba maazimio haya yanakwenda kidogo nje ya yale maazimio ya Umoja wa Afrika. Hasa ukitizama azimio nambari 1, 6 na 7.

Kwa maana hiyo Mhe. Spika, mimi mbali na kukubaliana na maazimio mengine yaani nambari 2,3,4,5,8, na 9, naomba haya maazimio nambari 1,6, na 7 tuyafanyie marekebisho kama inavyofuata.

Azimio nambari 1 Mhe. Spika na ukilisoma na azimio nambari 6. Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika ulisema kwamba zianzishwe mahakama maalum, lakini katika mkutano ule tulikubaliana kwamba kuna nchi nyengine zinaweza kufanya mahakama maalum na hasa Congo (Zaire) ilikuwa ndio moja katika hizo, kwa sababu kule matatizo hayo ni mengi sana kuliko kwetu sisi na matatizo haya yanakwenda mpaka hasa kwenye majeshi pale wanapoingia katika vita vyao. Majeshi wanafanya mambo haya ya kukamata watoto, na watu wazima. Kwa hivyo ile hali imekuwa mbaya zaidi.

Kwa hivyo, kule ndio kukaidhinishwa kwamba kwa nchi kama zile kuwe na mahakama maalum, hata wale wanajeshi. Lakini kwa nchi kama zetu ambazo matokeo yenyewe unaweza kupata kesi kama 5,10 au 20 uwe na kesi za vipindi kama nilivyosema.

Kwa hivyo, kifungu hiki namba 6 Mhe. Spika, badala ya serikali iwekeze rasilimali zaidi ili kuimarisha mahakama za watoto kwa kuweka idadi ya kutosha ya mahakimu wa kudumu, pale tuseme kwamba serikali iharakishe uanzishaji wa kesi za vipindi, ili kesi hizi zinapoanza ziweze kwenda mpaka zikamilike. Kwa hivyo, yale mambo ambayo napenda kushauri kuwa tuyabadilishe ni kama ifuatavyo:-

1. Serikali ihakikishe kuwa mkakati huu wa kitaifa ni endelevu na wote wanaohusika kwa kushirikiana na kamati ya kupambana na udhalilishaji wanaripoti serikalini kila baada ya muda.

2. Serikali ihakikishe kuwa vyombo vya habari vya serikali na vya binafsi vinatekeleza jukumu hilo la kutoa elimu juu ya janga hilo, kwa sababu na hili ilikuwa ni azimio moja la huo mkutano ambao ninauzungumza.

Mhe. Spika: Samahani Mhe. Waziri, hiyo ya 2 sasa ndio unakusudia ya 6 au ya 2, ni ipi sasa.

Mhe. Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Hapana, tunazifuta hizi ya 1, 6 na 7 kwa kuweka maazimio haya. Sasa ya tatu.

3. Wazee waelimishwe kuhusu ubaya wa suala hili na madhara yanayowapata watoto wetu na jamii kwa ujumla na kuhakikisha kuwa endapo mzee wa mtoto au yeyote anayehusika atapinga kutoa ushahidi au kutaka kesi yake ifutwe basi hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yake,

4. Kama nilivyosema kuhusu polisi, polisi waarifiwe na kuelimishwa kuwa kazi yao ni kupeleleza na kukusanya ushahidi na wao sio mahakama ya mwanzo au mahakama ya usuluhishi, wao wanatakiwa washirikiane na Ofisi ya DPP ili kupata muongozo mzuri wa kuendesha kesi hizo,

5. Serikali ihakikishe kuweka mahakama za vipindi yaani *session cases*, ili kesi za ubakaji zinapoanza ziendelee moja kwa moja mpaka zimalizike kwa kutolewa hukumu,

6. Mtuhumiwa wa kesi, hili Mhe. Spika, labda nilieleze kidogo. Katika azimio lile la Umoja wa Afrika, walisema watu wa aina hii wasipewe dhamana. Inajulikana kwamba dhamana ni haki ya kila mtu, lakini kikatiba na kisheria pale ambapo utasema kwamba kwa kesi hii mtu asipewe dhamana, itakuwa ndio imeshakubalika. Tukaombwa sote

tuliokuwa tunawakilisha nchi zetu, tuhakikishe kwamba sheria zetu zinasema kuwa mbakaji au muhalifu wa kesi hizi kwa matatizo haya, hapewi dhamana na inaendelea kesi yake wakati yuko kule kule mpaka kesi yake imalizike.

Kwa hivyo, na hii ndio nikasema tuiweke hapa kuwa sheria au mtuhumiwa wa kesi hii asipewe dhamana mpaka kesi yake imalizike na sheria zirekebishwe katika makosa ya jinai yanayohusiana na masuala hayo ili kukidhi matakwa ya maagizo ya Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika.

Mhe. Spika, hayo ndio mapendekezo ambayo tukiyaweka hapa, kwa kweli mapendekezo yetu yatakuwa yanalingana kabisa na yale maagizo ya Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika.

Mwisho Mhe. Spika, nilikuwa naomba tu katika hii *heading* ya azimio hili, hoja ya Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi ya Zanzibar kuliomba Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kutoa maazimio dhidi ya vitendo vya udhalilishaji wa watoto Zanzibar.

Sasa hapa mimi naomba tuongeze kidogo, kwa sababu lengo sio watoto tu, hata watu wazima wanawake katika nchi nyingi wanapata hujuma hizi. Kwa hivyo, hapa iwe ni udhalilishaji wa watoto na wanawake, au wanawake na watoto chini ya vifungu hivi alivyovitaja.

Baada ya marekebisho hayo Mhe. Spika, na mimi naunga mkono hoja hii moja kwa moja na naomba maazimio haya tuyakubali pamoja na marekebisho ambayo nimeyapendekeza. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuuchangia waraka huu ambao umechangiwa na wengi. Mimi ningependa nichangie kwa upande, sio kama mwanamke isipokuwa kama daktari na wanawake wanajua pakishatokea makosa wanasema na sisi tupo kwa hiyo bora niseme, nichangie kama daktari wa Kituo cha Afya Mnazi Mmoja, niende nikatafute taarifa, nione ule ukweli wa yale tunayoyasema ukoje na halafu tuweze kuyafikia maamuzi yatakayokuwa ya msingi.

Mhe. Spika, walichonieleza watu wa hospitali katika kitengo cha *One Stop Centre*, kwamba wao kama watu wa hospitali, kazi yao kubwa anapopelekwa mtuhumiwa au kujeruhiwa aliyefanyiwa kitendo cha ubakaji au kulawitiwa; Kwanza wanachotakiwa wachukuwe kipimo, halafu wamtibu majeraha, wampe dawa za *HIV* ili kumkinga, wamkinge na maradhi ya zinaa, wampe

dawa za kuzuwia mimba na mwisho wampe ushauri. Hayo ndio yanayofanywa katika kitengo hiki.

Lakini wakati huo huo kama madaktari wana njia nyengine moja ya kukusanya ushahidi wowote ule unaostahiki ambao utamsaidia mtu wa Mahakama kutoa uamuzi. Sasa kwa hadithi zilizopo hospitali ni kuwa watoto wengi walioulizwa ambao wamefanyiwa vitendo hivyo, ni kuwa wanafanyiwa vitendo hivyo kwa kitisho. Yule anayekifanya kitendo anamtisha mtoto kwanza na halafu ndio anakifanya kitendo kile.

Kwa hivyo, mtoto anaporudi nyumbani sio aghalabu ku-*report*. Wengi wa watoto hao wanaripotiwa au wanagunduliwa baada ya masaa kama 72 kupita. Asilimia 90 ya watoto walioripotiwa hapo walikwenda katika haki. Lakini hata wale waliowahi kwenda mapema wazee wao hawana elimu ya kutosha kuhusu jambo hilo. Mtoto akishafanyiwa hicho kitendo anamsafisha na kumkosha vizuri, anambadilisha nguo baadae anampeleka hospitali, wakifika pale ushahidi hakuna, kinachokutwa ni hayo majeraha. Kwa hivyo, wanachofanya ni kumtibu yule mtoto.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, hata wakisema wanataka wampelekee Jaji na Jaji pale kwa kuwa na yeye ni *layman* na yule kule aliyekwenda kuhukumiwa anasema bwana hapa hapana ushahidi, maana Unguja hakuna *DNA*, havijapatikana vithibitisho kwa sababu mbegu zangu hazikukutwa huko. Jaji anamuachia, anakwenda zake. Kwa hivyo, nyingi ya kesi zimekwenda kwa taratibu zote.

Mhe. Spika, lakini walipochunguza walikuta kwamba watoto wengi kati ya hao ni watoto ambao ndoa za wazazi wao zilivunjika. Aidha, baba anamg'ang'ania mtoto, sitaki watoto wangu, mama anaondoka peke yake anaolewa kwengine au mama anaondoka anasusa anawaacha watoto, watoto wanakuwa hawana malezi mazuri, wanahangaika hangaika na mwisho wake wanabakwa.

Kwa hivyo, suala la utulivu wa ndoa na wazazi kukaa pamoja ni silaha kubwa itakayowalinda watoto wetu wasibakwe, kwa sababu asilimia kubwa ya watoto hao waliobakwa utakuta labda anakaa na shangazi, mjomba, ilimradi hawana utulivu katika familia kila wanapokaa wanahangaika mwisho wake yanawakuta yanayowakuta.

Jengine ambalo wameniambia ni kwamba polisi ili *DNA* iweze kufanyika, basi kuna mambo yanatakiwa yapatikane kwa upande wa aliyefanyiwa kitendo na yule mfanyaji wa kitendo. Mara nyingi polisi hawapeleki hospitali,

ili waweze kuchukuliwa hivyo vipimo viweze kulinganishwa katika hiyo *DNA* inayotakiwa kupimwa.

Kwa kipindi chote hicho cha miaka mitatu walichokuwa wanakusanya *data*, ambapo watoto wengi walifanyiwa vitendo vilivyokuwa havina maana, watu 3,296 waliripoti kwenye kituo. Katika watu 3,296 watu waliopatikana wanaume ni wawili tu. Sasa hiyo *DNA* tunayokaa tukaidai itafanyiwa vipi. Kweli tuweke *DNA machine* kwa watu wawili, watu 3,296 au tuseme 3,300 ni wanaume wawili tu, sasa kazi hiyo itafanyika vipi.

Lakini hata hivyo, chengine kinachojitokeza na wanachokisema watu ambacho mimi sina ushahidi nacho ni kwamba polisi na mahakama rushwa imezidi, ndiko kunakoharibiwa mambo. Wakienda kule watu wenye pesa zao wanalipa na polisi kwa njaa zao na watu wa mahakama hawashibi, wanachukua rushwa halafu wanapinga haki, hawa watu hawapewi haki zao. Sasa sijui kama na mishahara ya polisi na watu wa mahakama irekebishwe ili jambo hilo likome. Lakini hayo yanasemwa na watu, sina ushahidi nayo.

Pia, Mhe. Spika, kinachojitokeza zaidi, polisi wakati wa kuchukua uthibitisho, uthibitisho ule unatakiwa ufungwe vizuri uwe *sealed*, kama vile barua ya siri inavyofungwa, ili kipimo kile kiende moja kwa moja mpaka kwa mkemia, mkemia apokee kikiwa kimefungwa na ahakikishe kwamba kweli hakikufanyiwa mambo mengine yasiyofaa. Lakini *handling* ya hivyo vipimo kwa kweli polisi sijui kama hawana ujuzi wa kutosha, lakini *handling* yao ya *spaceman* sio nzuri. Kwa hivyo, kunatokea sababu tele za kusababisha ushahidi usipatikane.

Mhe. Spika, sasa mimi nafikiri tuzungumzie nini kosa, hapa wengi wetu tunazungumzia *DNA*. Tunajua kama si mtu wa sayansi ya kidaktari tunazungumza tu suala la *DNA* hatujui tunachokizungumza ni kitu gani. Labda niwape uelewa kidogo wenzangu tufahamiane. *DNA*, sitaki niseme kizungu changu, lakini ni kipimo ambacho kinapima vinasaba. Tunapozungumza vinasaba tunataka tuelewe ukoo unakwendaje. Mimi nimezaliwa na baba yangu natakiwa nikipimwa, *DNA* ilingane kwa kiasi fulani na mama yangu, ilingane kwa kiasi fulani na baba yangu. Kwa hivyo, hapo ninakuwa mtoto halali wa wazee wale wawili.

Lakini ukimpima mtoto ukikuta analingana na mama yake na atalingana naye kwa sababu mama ni mwanawe. Lakini baba akiwa sio yule hutokuta ule uasilia wa yule mtoto. Kwa hivyo, mtoto huyo atakuwa kapewa tu baba yule, lakini si baba halali kwa vinasaba vile. Mara nyingi tunapima vipimo kama hivyo pale watoto walio chini ya miaka 18 wanapopata ujauzito, anapopata ujauzito mara nyingi kwa kubakwa, anaposema kwamba mtu fulani ndie

aliyenibaka inabidi sasa tusubiri, kama ingekuwa nchi zilizoendelea kipimo kinaweza kufanyika wakati mjamzito wanamtoa maji ya kwenye fuko la uzazi wanapima.

Anapimwa damu baba mtu na mama mtu, unaweza ukapata jawabu hata kabla mtoto hajazaliwa, kama huyu wake au sio wake. Lakini kwetu sisi hatujafikia hivyo, hata hapo Tanzania Bara hawajafikia, kinachofanyika inabidi asubiriwe mtoto azaliwe atolewe damu, pamoja na mama na baba watolewe damu na wende wakafanye uchunguzi kuangalia kwamba je mtoto huyu ana nasaba na wazazi husika. Hiyo ni moja.

La pili, *DNA* inatumika panapotokea kesi za mauaji (*criminal cases)* hilo linakuwa zaidi jepesi kwa polisi, kwa sababu tuseme mfano mtu kachomwa kisu, aliyechomwa kisu damu zikichirizika ikimdondokea yule mchomaji na yule akimtambua kwamba ndie aliemchoma, ikichukuliwa hata kama damu imekauka ikipimwa itakutikana kwamba damu ile iliyokutikana kwenye nguo ya mtu yule na damu ya yule aliyefanyiwa kitendo kile inafanana. Sasa hizo ni ulinganifu wa damu ile na ile. Hicho ni kipimo cha pili.

Kipimo cha tatu kikubwa ambacho kinafanyika katika nchi zilizoendelea ni kwa ajili ya Jumuiya kwa ujumla ya nchi ile, wanaita *public*. Wenzetu walioendelea nchini kwao kuna *data base,* kila mtu anajulikana damu yake na vinasaba vyake, kama kunatokea ajali kubwa au mtu kafariki hakujulikana vimekutwa tu vitu vya mwisho hata kama ni mfupa basi huo mfupa unaweza ukachukuliwa ukapimwa na wanakwenda kwenye *library* yao wanatafuta na wanamjua huyu ni mtu gani. Hizo ni nchi zilizoendelea, hapa kwetu kama yatafika si leo wala kesho.

Matumizi makubwa ya *DNA* yanatumika kwa utaratibu huo, kwa mfano ikitokea ajali kubwa ili kuweza kutambua nani ndio nani wanaweza kutumia *DNA*. Hapa kwetu na hata ukienda Tanzania Bara ukitaka kusema tu mimi nataka nimjue kama huyu mwanangu au sio mwanangu, lazima kwanza wapate ruhusa kutoka kwa mahakama iwaambie kwamba fanyeni hivyo, bila ya hivyo hawapimi. Kwa hivyo, hizo ndizo *DNA* zinavyotumika.

Sasa tuangalie kwa hapa kwetu katika watu 3,300 watu wawili tu ndio walioweza kupelekwa wakapatikana na makosa na hawakupelekwa wenyewe na polisi. Kuna kesi mbili, kesi ya kwanza mtoto mdogo alibakwa, alichukuliwa kwenye nyumba na mtu akamfanyia vitendo hivyo.

Kwanza yule mtoto alipokwenda kule alikwenda na viatu, kwa fadhaa zake baada ya kukurupuka mule ndani akaviacha viatu ndani. Alipokwenda kushtaki kwao, akaulizwa ni nani, akamtaja akasema na nyumba

aliyopelekwa. Alipoulizwa kulikuwa kuna nini, akasema yule bwana alimchukua akachukua chupa ya malta akanipaka, akajipaka na yeye kisha akanifanyia vitendo hivyo, akaniambia itakuwa haiumi.

Kwa hivyo, wakenda, walipokwenda na polisi kweli chupa ya malta ilikutikana humo ndani na viatu vya mtoto vilikutikana humo ndani. Sasa kuna ushahidi zaidi ya huo wa kwamba mtu huyo asichukuliwe hatua. Alichukuliwa akapelekwa *One Stop Centre*. Polisi walichokifanya kitu cha kwanza vile viatu ambavyo ni ushahidi wakampa mtoto avae viatu vyake, aende zake na ndio ushahidi uliokutikana ndani na chupa ilikutikana ndani.

Lakini mpaka leo watu wa *One Stop Centre* hawajui kesi hiyo ilikwishia wapi, ambayo ndio ilikuwa ina ushahidi kamili wala haihitaji *DNA*. Mtoto yule alikutwa, ni katika hao watoto watano ambao nawasema na yeye alikutwa tayari na hizo mbegu za kiume alipofanyiwa, lakini hawakupata haki yao mpaka leo.

Kesi ya pili ambayo mtoto mwanamke ana miaka 17, kikundi cha watoto wa kiume walimzingira wakamkamata wakataka kumchangia. Sasa wakawa wanafanya mmoja baada ya mwengine. Huyo mmoja ambae ndie aliyekamatwa hapa tunayemzungumzia alipokuwa anafanya yale akamwambia yule mtoto wa kike ninyonye na ulimi, yule mtoto wa kike akamwambia ulete, akautafuna mpaka akaukata, alipoukata ule ulimi akakurupuka yule bwana na wenziwe wakakimbia kwao akachukuliwa mtoto yule akapelekwa Al-Rahma, akawaambiwa hapana hii sio kesi yetu, hii itabidi mumpeleke Mnazi Mmoja.

Kwa bahati nzuri na yule mtoto wakati huo huo akapelekwa Mnazi Mmoja na *One Stop Centre*, walipokwenda kuuliza *OPD* wakaambiwa kuna mtoto ambaye ni mwanamme mzima, baleghe kakatwa ulimi na yuko kwenye wodi ya wafungwa kule yuko chini ya ulinzi.Wazee wa mtoto mwanamme walitaka kumtorosha, lakini akawahiwa akawekwa chini ya ulinzi na hiyo kesi mpaka leo haikupata hukumu. Je, kunatakiwa *DNA* gani kwa hilo.

Mhe. Spika, hizo ndizo kesi mbili ambazo zinatambulikana. Mimi naijua kesi ya tatu na hii mara nyingi inawapata watoto wale wenye akili taahira. Mtaani kwetu kulikuwa na mtoto tahira, alikuwa anafungwa minyororo na wazee wake na kuna bwana mmoja jirani yake pale akiitwa babu Komba. Kama watu wa zamani mlikuwa mnatazama TV, yule mtoto akapata ujauzito, wazee wake wakawa wanajiuliza, huyu mtoto kila siku anafungwa ndani tena kwa minyororo ujauzito kaupataje.

Mtoto taahira, lakini tahira hasemi uongo wale wanasema ukweli, kwa sababu hata huko kutunga uongo hawajui, kutokana na zile akili zao. Akasema mimi hapa kila siku babu Komba anakuja akinilalia, matokeo yake ndio hayo. Lakini wakati ule kesi zilikuwa sio kama hivi ambavyo leo hii tunazizungumza. Wazee wakanyamaza kimya wakapata mjukuu wao, wakaendelea kumlelea.

Lakini hayo yanajulikana, babu Komba kamlalia sio mara moja, sio mara mbili, sio mara tatu. Sasa tunataka ushahidi upi. Ili ifanyike *DNA* ambapo kuna watu wawili kati ya watu 3300. Hayo ndio yanayotokea katika mitaa. Sasa akipelekwa mtoto bubu korti, wanasema kwamba huyu hawezi kusema hata kama mkalimani kenda, wanasema hawezi kutoa ushahidi. Kwa hivyo, wao wanakuwa hawapati haki pia. Sio bubu mmoja, sio wawili ambao wamefanyiwa hayo na wamekosa haki zao kwa sababu eti hawasemi.

Sasa kama ni hivyo na kama kesi itakwenda hivyo basi hata siku moja haipatikani haki. Ukenda polisi mtoto kabakwa, akiwa mjamzito ukimpeleka tu wanasema kwanza sisi hatushughulikii mimba hapa. Sisi tunashughulikia watu waliobakwa. Sasa jamani kama mtu anamjua na mimba anayo kwa nini sasa hao polisi wasisubiri wakachukua hizo *DNA* wakapeleka. Mimi Nafikiri polisi nako kuna matatizo, kwa sababu sisi tunafanya nao kazi na kwa Mkemia Mkuu.

Ile kulipa hawataki, maana vipimo vyao vyote wanapeleka pale. Mpaka tulipowaandikia barua Wizara ya Afya tukawaambia tutakuwa hatuwapimi tena. Ndio wameanza sasa hivi kutulipa kidogo kidogo, sikuambii kuchukua vipimo wakaenda navyo Dar es Salaam, ina maana ni gharama kubwa zaidi. Kwa hivyo, hakuna kipimo kinachochukuliwa kwenda Dar es Salaam kwenda kupimwa.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, mnaotoka nje sio muda mrefu kuanzia sasa tutapitisha hoja hii, *quorum* yangu itapotea naomba murudi tumalize shughuli hii. Mhe. Naibu Waziri endelea.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, tatu, kwa utaratibu huu mimi naona tuzungumze hapa, lakini kwa mwenendo huu tunaokwenda kama majaji na polisi hawakubadilika hata Wizira ya Afya, *One Stop Centre* wakifanya watakavyofanya haitosaidia. Mimi huwa nasikiliza sana magazeti ya asubuhi, kila siku utasikia Shinyanga kafungwa mtu miaka 30, Bariadi kafungwa mtu miaka 30, kule *DNA* mashine hazipo, lakini watu wanafungwa kutokana na ushahidi wa daktari.

Leo hii hata daktari kama yupo, *report* ipo pale, ikipelekwa korti jaji anasema mimi siwezi kuhukumu na kama huyo aliyechukua ushahidi huo hayupo kesi anafuta. Sasa tutafika wapi.

Lakini chengine nilichokikuta kikubwa huko katika mabuku ya daktari si watoto tu na wanawake kupigwa, jamani kila siku au kila mwezi udhalilishaji wa wanawake upo na unaendelea. Wanawake wanapigwa kwa mwezi kesi 30 mpaka 40, wanapigwa na waume zao wanakwenda Mnazimmoja hospitali. Kwa hiyo, hawadhalilishwi watoto tu kwa kubakwa na wanawake pia wanadhalilishwa kwa kupigwa na waume zao.

Watoto pia wanapigwa na walezi, wale ambao wasiokuwa na walezi ambao ni baba zao na mama zao mara nyingi kesi zipo kule, wanapigwa vibaya sana, na wanaumizwa. Wenzetu Bara mara nyingi utaziona kesi kama hizo kwenye *TV* lakini na hapa Mnazi Mmoja zipo, ingawa hakuna hata mtu mmoja anayechukuliwa hatua.

Mimi nasema hapa kwamba unyanyasaji wa watoto upo kwa kiasi kikubwa na haki watoto hawatendewi kwa sababu wazazi wanakuwa hawana elimu, baada ya tukio wanamsafisha mtoto wakimpeleka hospitali inakutikana hakuna ushahidi. Ule ushahidi wowote wa ule ubovu wa yule mtoto jaji hautilii maanani kwa sababu anasema anaweza akatenda yoyote hata kama mtoto atasema huyu ndiye aliyenifanyia hivi.

Kwa mantiki hiyo Mhe. Spika, mimi naomba nimalizie hapa nafikiri sasa jamii ielimishwe ili watoto wafikishwe hospitali kwa wakati bila yakusafishwa. Lakini na ile *attitude* ya polisi na majaji ibadilike ili tupate haki. Vyenginevyo tutadai *DNA* ambayo ndiyo kwanza mashine sasa hivi tunayo moja, nyengine inataka milioni 600, tunatakiwa tujenga hiyo maabara yenyewe, tutafika lakini si leo wala kesho.

Mhe. Spika: Sasa baada ya kumaliza mjadala huu naomba sasa nimkaribishe Mhe. Mwenyekiti, muongozo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nilikuwa nataka nisaidiwe ufafanuzi kidogo, kwa sababu tulivyokuwa tukijenga hoja hii ya udhalilishaji hasa wa watoto, wajumbe wengi tulikazania kwamba serikali katika bajeti inayokuja kuhakikisha kwamba mashine ya *DNA* inapatikana. Lakini kutokana na mchango wa Mhe. Naibu Waziri wa Afya, imeonekana kwamba hata hiyo mashine ya *DNA* ikipatikana bado kuna udhaifu katika maeneo mengine kwa hawa ambao watakaochukuliwa hizo *DNA.*

Lakini kwa kuwa tatizo tunaloliona kama alivyozungumza Mhe. Waziri, wa Katiba na Sheria katika mchango wake, katika hizi kesi za watoto lazima turekebishe sheria ya kuweza kutokuwapa dhamana hawa wahusika na ndio itakayosababisha hawa wanaotaka kutolewa hizo *DNA* waweze kupatikana ambavyo sasa hivi sheria hiyo haipo. Kwa hivyo, bado Mhe. Mwenyekiti, kabla ya mtoa hoja hajenda kutoa maelezo yake nilikuwa nina wasi wasi asijeakaona ile hoja tuliyoijenga ya kupatikana *DNA* akaja akaona kwa udhaifu uliokuwepo itakuwa haina maana. Bado nilikuwa naomba sana Mhe. Spika, umuhimu wa kupatikana *DNA* upo.

Lakini vile vile, kupitia azimio hili nadhani Mhe. Mwanasheria Mkuu yupo, sisi sote tumeshaona ni maeneo gani ambayo yana udhaifu katika sheria, kwa hiyo tunategemea katika kikao kitakachokuja atatuletea katika yale marekebisho ya sheria mbali mbali, haya yote ambayo tumeyaona yana matatizo tuweze kuja kuyafanyia marekebisho ili hili suala la udhalilishaji wa watoto tuweze kulikomesha kabisa.

Mhe. Spika, hiyo ndio ilikuwa hoja yangu.

Mhe. Spika: Sasa unamtaka Spika aongoze nini hapo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, sio muongozo zaidi ilikuwa ni hoja.

Mhe. Spika: Nafikiri tumuache mtoa hoja atoe maelezo yake, Baraza tutaamua kama hiyo mashine ya *DNA* iweze kununuliwa katika wakati gani muwafaka, hiyo ni kazi yetu sisi.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Spika, awali ya yote nichukue fursa hii adhimu kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma, aliyetujaaliwa kufika hapa tukiwa wazima wa afya na kuweza kuendelea na shughuli zetu ambazo zimetuletea hapa. Pili nikushukuru wewe kwa kunipa tena fursa hii ya kuja kuweza kuleta hoja yangu mbele ya Baraza lako tukufu na kuweza kufanya majumuisho.

Mhe. Spika, kiujumla wajumbe wote ambao wamechangia hoja hii walikuwa 28. Mhe. Spika, kwa ruhusa yako nakuomba niwataje waliochangia katika hoja hii.

1) Mhe. Hamza Hassan Juma
2) Mhe. Ismail Jussa Ladhu
3) Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
4) Mhe. Suleiman Hemed Khamis

5) Mhe. Wanu Hafidh Ameir
6) Mhe. Marina Joel Thomas
7) Mhe. Panya Ali Abdalla
8) Mhe. Salmin Awadh Salmin
9) Mhe. Muhamed Raza Hasanali
10) Mhe. Husein Ibrahim Makungu
11) Mhe. Hija Hassan Hija
12) Mhe. Hassan Hamad Omar
13) Mhe. Jaku Hashim Ayoub
14) Mhe. Asaa Othman Hamad
15) Mhe. Salim Abdalla Hamad
16) Mhe. Salma Mussa Binali
17) Mhe. Amina Iddi Mabrouk
18) Mhe. Kazija Khamis Kona
19) Mhe. Rufai Said Rufa
20) Mhe. Waziri, Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto
21) Mhe. Mwanasheria Mkuu
22) Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria
23) Mhe. Naibu Waziri wa Afya

Mhe. Spika, pia kuna ambao wamechangia kwa kutumia maandishi. Naomba Mhe. Spika, uniruhusu niwataje na hao.

1. Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
2. Mhe. Farida Amour Muhammed
3. Mhe. Ashura Sharif Ali
4. Mhe. Fatma Mbarouk Said
5. Mhe. Ussi Jecha Simai

Mhe. Spika, baada ya kuwaorodhesha wajumbe waliochangia naomba sasa nitoe maelezo ya hoja za Wajumbe kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba niwashukuru wajumbe wote ambao wamechangia na kuunga mkono hoja hii kwa hisia kubwa. Na wengi wao wametoa mifano mbali mbali hasa inayokwaza utekelezaji wa haki za mtoto katika jamii na taasisi zinazoshughulikia kutoa haki katika kesi za udhalilishaji wa watoto.

Mhe. Spika, kwa kuwa hoja yangu niliyoileta ilikua ni kuomba ridhaa ya Wajumbe wa Baraza lako kuyakubali maazimio tisa (9) ambayo yataweza kushughulikia usimamizi wa mambo yote yanayohusiana na kesi za udhalilishaji wa Watoto. Katika michango ya Waheshimiwa Wajumbe nimeona niigawe kwa mujibi wa hoja walizochangia na kutokana na kila

azimio. Wajumbe wote waliweza kuunga mkono maazimio yote niliyokuja nayo huku wakitoa msisitizo kwa baadhi ya maazio.

Mhe. Spika, azimio namba moja hili liliungwa mkono na Wajumbe wote wa Baraza na kutaka kuwepo kwa vikao kati ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mkurugenzi wa Mashtaka na Waziri wa Katiba na Sheria kwa lengo la kutafuta suluhisho la vitendo vya udhalilishaji kwa watoto. Vile vile, katika azimio hili Mwanasheria Mkuu aliwaomba Wajumbe wa Baraza kuwa wao waunde umoja ambao utakuwa unaweza kusaidia masuala yote ya udhalilishaji wa watoto.

Mhe. Spika, azimio namba mbili nalo limeungwa mkono na Wajumbe wote na kuitaka Serikali kwa bajeti inayofuata 2014/2015 na zaidi ya hapo kuwekwa kifungu cha fedha zitakazoweza kusaidia katika utekelezaji wa hatua za kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa watoto. Ambapo azimio hili limeungwa mkono sana na Mhe. Salmin Awadha Salmin, Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Mhe. Hija Hassan Hija.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu, yeye katika azimio namba tatu alipendekeza liongezewe maneno au kuwepo na azimio jipya litakalosomeka,

> "Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo vipitie vipindi ambavyo vinarushwa katika vyombo vya habari pamoja na matamasha na kuhakikisha kuwa vinakwenda sambamba na maadili yetu ya kizanzibari"

Lengo la azimio lake ilikua ni kusaidia katika kuyahifadhi maadili yetu pamoja na kupunguza kasi ya ongezeko la vitendo vya udhalilishaji. Mshe. Spika, ushauri wa Mhe. Ismail Jussa Ladhu nimeukubali na nauchukua ushauri huu kama ni azimio jipya katika haya ambayo nimeyaleta mbele ya Baraza lako.

Mhe. Spika, katika azimio la nne Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Rufai Said Rufai, Mhe. Salim Abdalah Hamad na Mhe. Salma Mussa Bilal wote kwa pamoja wamekubaliana na azimio namba nne na wameomba suala la kuelimisha jamii lizingatiwe katika ngazi zote.

Mhe. Spika, katika azimio la tano nalo limechangiwa na kuungwa mkono na Wajumbe takriban wote kati ya hao ni Mhe. Kazija Khamis Kona, Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Salma Mussa Bilal, Mhe. Amina Iddi Mabrouk, pamoja na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, ambao wote kwa pamoja walitilia mkazo kuingizwa elimu ya udhalilishaji katika mitaala.

Mhe. Spika, katika azimio la sita Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria amesisitiza katika mapendekezo yake ambapo kutokana na mkutano wa Jumuiya ya Afrika ambao ulifanya maamuzi ya kuwepo mahakama ya watoto kuimarisha mahakama zetu na kuwepo na *session cases* ambazo zitasaidia katika utekelezaji wa utolewaji wa maamuzi kwa muda mfupi.

Mhe. Spika, kwa upande wa azimio namba saba Wajumbe wengi wamekubaliana na azimio hili na kutaka serikali iifanyie mapitio sheria ya mtoto.Vile vile, Mhe. Hamza Hassan Juma, katika azimio hili ameshauri kuwa suala la udhalilishaji lisiachiwe serikali peke yake hasa katika kuleta miswada na badala yake Wajumbe, *NGOs*, na taasisi mbali mbali zina uwezo wa kuleta miswada Barazani na hivyo tutaweza kuisaidia sana serikali katika kulifanyia kazi suala la udhalilishaji.

Mhe. Spika, azimio namba nane limeungwa mkono na Wajumbe wote wa Baraza ambao kwa pamoja wameitaka serikali kuhakikisha kuwa kifaa cha *DNA* kinapatikana ndani ya muda mfupi kwa lengo la kuondoa changamoto iliyopo sasa kwa kukosekana kwa kifaa hiki ambapo kesi nyingi za udhalilishaji hazipatiwi ufumbuzi.

Vile vile, Mhe. Amina Iddi Mabrouk nae kwa upande wake alipendekeza kutokana na kuongezeka kwa mimba za utotoni kifaa cha *DNA* kitaweza kusaidia katika kuwatambua wahusika wa matukio hayo.

Mhe. Spika, azimio la tisa nalo Wajumbe wote wameliridhia na wameona kuna haja kwa serikali kutoa *report* dhidi ya vitendo vya udhalilishaji kwa kila mwaka pale ambapo itatolewa *report* ya mtoto inayotolewa na Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii,Vijana na Watoto.

Mhe. Spika, vile vile, napenda nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii,Vijana na Watoto kwa kuunga mkono hoja pamoja na kutoa ufafanuzi wa kina juu ya hatua zinazofanywa na Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii,Vijana na Watoto.

Mhe. Spika, Wajumbe wamelizungumzia suala la rushwa ambalo nalo linachangia kwa kiasi kikubwa katika kuendeleza vitendo vya udhalilishaji ndani ya jamii yetu na kuitaka jamii nzima kushirikiana katika kuhakikisha suala hili linapigwa vita la kupatikana haki katika maamuzi ya kisheria.

Mhe. Spika, pia, suala la upatanishi unaofanywa na wazee pamoja na wafanyaji wa vitendo vya udhalilishaji katika kumaliza kesi kimaafikiano bila kufika katika sehemu za mahakama, wajumbe wote wamelipigia vita na

kutaka kuwekwa kwa sheria ambayo itamchukulia hatua mzee yeyote atakaekubaliana na suala hilo.

Mhe. Spika, kabla ya kumaliza majumuisho yangu naomba nikubaliane sana na Mhe. Waziri wa Sheria na Katiba katika marekebisho ambayo ameyafanya ya kifungu Nam 1, 6, 7. Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba kusema kwamba pamoja na marekebisho hayo nimeyakubali na nimeyaafiki.

Mwisho kabisa napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wote ambao waliochangia, wamechangia kwa dhati na nawashukuru sana na nawapongeza kwa michango yao. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mgeni Hassan Juma, tunakushukuru sana kwa majumuisho hayo uliyoyafanya kwa ufundi mkubwa, kwa kipindi kifupi sana. Hii inathibitisha yale maneno ambayo Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliyoyazungumza mapema wakati wa mchana. Kwa hivyo, baada ya hayo, sasa Waheshimiwa Wajumbe naomba niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hii pamoja na maazimio yake na marekebisho mbali mbali yaliyofanywa katika ukumbi huu wanyanyue mikono, waliokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Baada ya kazi hii kuifanya, hili jambo ni jambo la mtambuka, kwa hivyo kwa kawaida mambo yote yale ya mtambuka huwa tunayapeleka kwa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Kwa hivyo, Makatibu wangu wakishakuweka vizuri marekebisho mbali mbali ya maazimio haya pamoja na yale maazimio mengine ambayo yamependekezwa na Mtoa hoja ameyakubali kama alivyopendekeza Mhe. Ismail Jussa Ladhu, basi tutayaelekeza Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na yeye ataandaa utaratibu sasa kila mwenye suala lake katika Wizara husika liweze kufanyiwa kazi.

Lakini pia, Mhe. Mwanasheria Mkuu mtakumbuka alipendekeza kwamba Baraza lenyewe nalo lichukue nafasi katika jambo hili. Pia, mtoa hoja jambo hili alikubali na sisi kama uongozi tutaandaa utaratibu ili kuona namna gani ya kutengeneza hiyo kamati iliyopendekezwa. Kamati ambayo tutaitafutia fedha ili tuitume katika jamii yetu, maeneo mbali mbali kutoa taaluma ya mambo haya ya kusisitiza na kuonesha kwa wananchi kwa kiasi gani jambo hili chombo chetu cha kutunga sheria, serikali na jamii nzima linatuchukiza. Jambo hilo tayari tumekwisha kulikalia kitako hata kabla ya kufanya majumuisho haya.

Basi waheshimiwa wajumbe baada ya hayo nikushukuruni na sasa Katibu tunaendelea. Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, kuna maneno.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri kwa mujibu wa Kanuni kwa sababu haya maazimio ni mengi inatakiwa kila mmoja uulize kama limekubaliwa au halikukubaliwa.

Mhe. Spika: Unajua nimeiona hiyo Kanuni ya 48(5)(c) ila kwa sababu ya maelezo aliyotoa mtoa hoja na kutokana na marekebisho mbali mbali ambayo kwa bahati nzuri ameyataja, uliyoyatoa mwenyewe, aliyoyatoa Mhe. Ismail Jussa Ladhu, pia na yale ambayo yamependekezwa na Mhe. Mwanasheria Mkuu, ndio nikayachukua kwamba maazimio haya pamoja na marekebisho yake. Marekebisho yamo kwenye *Hansard* na Katibu atayafuata na sasa hayo tutaweza kuyaweka kwa pamoja na kuyaelekeza kwenye Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Sheria ya Hati Miliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo

(*Kusomwa kwa mara kwanza)*

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati Kny/Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria ya kuanzisha Sheria ya Hati Miliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo kusomwa kwa mara ya kwanza.

Mswada wa Kufuta Sheria ya Karafuu Nam. 11 ya Mwaka 1985, na Kuweka Sheria Mpya ya Maendeleo ya Karafuu na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo

(Kusomwa kwa mara ya kwanza)

Mhe. Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko: Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Kufuta Sheria ya Karafuu Nam. 11 ya mwaka 1985, na Kuweka Sheria Mpya ya Maendeleo ya Karafuu na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Kusomwa kwa mara ya kwanza.

Mswada wa sheria ya Kuanzisha Shirika la Nyumba Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo

(Kusomwa kwa mara ya kwanza)

Mhe. Waziri Ardhi, Mkaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa sheria ya Kuanzisha Shirika la Nyumba Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Kusomwa kwa mara ya kwanza.

Mhe. Spika: Miswada hiyo imesomwa kwa mara ya kwanza na kwa maana hiyo iko tayari kufanyiwa kazi na Kamati.

Baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe naomba sasa nimkaribishe kwa heshima kubwa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais. *(Makofi)*

KUAHIRISHA BARAZA

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais:

Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uzima, afya njema na utulivu na pia kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu tuliyojipangia katika Mkutano huu wa Kumi na Nne kwa salama na amani. Pili, nikushukuru wewe Mhe. Spika pamoja na Wasaidizi wako wote kwa umakini, busara na hekma zilizopelekea kuendesha Mkutano huu wa Baraza la Wawakilishi kwa ufanisi mkubwa sana.

Mhe. Spika, vile vile napenda niwashukuru Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Baraza kwa kuziongoza Kamati zao na kutekeleza majukumu yao vyema.

Mhe. Spika, kwa dhati kabisa nimpongeze Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kuiongoza nchi yetu kwa umakini na kuweza kupata mafanikio makubwa. Ushauri na miongozo

yake kwetu inatusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu, kwa manufaa ya nchi yetu na wananchi wote.

Mhe. Spika, aidha, nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa majadiliano mazuri na ushauri wenye kujaa busara na hekima wenye nia ya kuimarisha utendaji na utekelezaji wa majukumu yetu ya kila siku. Pia, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri kwa kutoa ufafanuzi wa kina wa hoja mbali mbali zilizoulizwa na Waheshimiwa Wawakilishi kwenye mkutano huu.

Mhe. Spika, mnamo tarehe 5 Disemba, 2013 Bara letu la Afrika na ulimwengu kwa jumla ulipata msiba mkubwa na usioweza kusahaulika wa kuondokewa na kiongozi shupavu, mvumilivu na mtetezi wa haki za binaadamu wote na mkombozi wa wananchi wa Afrika ya Kusini, Mheshimiwa Mzee Nelson Mandela.

Ni wazi kwamba kiongozi huyu aliepigania uhuru katika nchi yake ya AfrikaKusini hatosahaulika kwa kuionesha dunia utu wa hali ya juu kwa kuweza kusamehe na kusahau yaliyopita na kuwataka wananchi wote wa Afrika Kusini kushirikiana bila ya ubaguzi wa dini, rangi au ukabila. Mzee Mandela hakuwa mtu wa kulipa kisasi kama wengi wangeweza kufikiria.

Mzee Mandela ameutumia umri wake wote wa ujanani kwa jela ambako alifungwa kwa muda wa miaka 27.

Mhe. Spika, bila shaka tuna mengi ya kujifunza kutokana na maisha ya Mzee Nelson Mandela katika kujali utu, kusamehe, uvumilivu na moyo wa kuipenda nchi na Bara letu na kuwa na mahusiano mema na binaadamu wote katika dunia. Mzee Mandela aliwasamehe waliomfanyia uovu huo, pamoja na kuamini kuwa Mungu hakumuumba mtu muovu ila uovu ni wa mtu mwenyewe. *(Makofi).*

Mhe. Spika, kama sote tunavyoelewa kwamba, kila ifikapo tarehe 12 Januari ya kila mwaka, nchi yetu inaadhimisha sherehe za Mapinduzi yetu Matukufu yaliyotokea mwaka 1964. Ifikapo tarehe 12 Januari, 2014 Mapinduzi hayo yatatimiza miaka 50.

Mhe. Spika, kwa ujumla Maadhimisho haya yaliyozinduliwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tarehe 15 Agosti, 2013 yanaendelea vizuri. Tangu yalipozinduliwa tumeshuhudia wananchi wakisherehekea kwa kufanya usafi wa mazingira, kushiriki katika matamasha mbali mbali ya michezo na burudani pamoja na uzinduzi, uwekaji wa mawe ya msingi na ufunguzi wa miradi mbali mbali ya maendeleo. Nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wazidi kuhamasisha wananchi kuendelea kushiriki kwa wingi katika matukio mbali ya sherehe hizi pamoja na siku ya kilele hapo Uwanja wa Amaan, tarehe 12 Januari, 2014.

Napenda kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote waliopangiwa kuzindua au kuweka mawe ya msingi kwa miradi mbali mbali ya maendeleo kwa kuifanya kazi hiyo vizuri na kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika, katika kusherehekea miaka 50 ya Mapinduzi, Serikali imeandaa maonesho yatakayofanyika katika viwanja vya Beit al Ras kwa siku nne kuanzia tarehe 2 Januari, 2014 hadi tarehe 5 Januari, 2014 ambapo Taasisi za Serikali, Taasisi Binafsi na Jumuia za Kiraia watapata fursa ya kuonesha shughuli zao wanazozifanya, huduma wanazozitoa au bidhaa wanazozalisha. Hii ni fursa ya pekee kwa wananchi wa Zanzibar pamoja na wageni kutembelea kwenye maonesho haya ili kuona mafanikio yetu ya miaka 50 tangu kufanyika kwa Mapinduzi ya Januari 12, 1964.

Mhe. Spika, sote tunaelewa kwamba Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Awamu ya Tatu (*TASAF III*) tayari umeshaanza shughuli zake hapa Zanzibar na imeshafanya shughuli nyingi zikiwemo kutoa mafunzo ili kujenga uelewa wa lengo la *TASAF* Awamu ya Tatu kwa wadau mbali mbali tukiwemo Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu. Aidha, kaya maskini tayari zimeanza kutambuliwa kwa mashirikiano na wanajamii wenyewe. Kwa Unguja jumla ya kaya maskini 2,500 zimetambuliwa na kwa Pemba hadi sasa jumla ya kaya 4,000 zimeshatambuliwa.

Kazi ya kuzitambua kaya maskini inaendelea kwa Shehia zote za Unguja na Pemba. Aidha, hatua ya kuzihakiki kaya zilizokwisha tambuliwa zimeanza na tunatarajia kuanza kutoa malipo kwa kaya hizo ifikapo mwezi Januari, 2014. Nachukua nafasi hii, kuwaomba Waheshimiwa Wawakilishi kuendelea kutoa ushirikiano katika zoezi zima la kuzitambua na kuzihakiki kaya maskini ili malipo yaweze kufanyika kwa wale wanaostahiki na si vyenginevyo.

Mhe. Spika, bado tumo katika kipindi cha mvua za vuli na katika kipindi cha hivi karibuni tumeshuhudia kupatikana kwa mvua kubwa katika baadhi ya maeneo. Kutokana na mabadiliko ya tabianchi na athari zake kuikumba dunia, ni vyema kwa taasisi zote zinazohusika kufuatilia mwenendo wa hali ya hewa

na kutoa taarifa za mapema kwa wananchi hususan wakulima na wavuvi na wanaosafiri kwa kutumia usafiri wa angani na baharini ili kuchukua tahadhari na kupanga vyema shughuli zao.

Mhe. Spika, Sekta za Kilimo na Maliasili bado zinaendelea kuwa ni muhimili mkuu wa uchumi wa Zanzibar ambapo inatoa mchango wa moja kwa moja katika kujikimu kimaisha, kuwa na uhakika wa chakula, lishe na afya za wananchi walio wengi vijijini na mijini. Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 sekta hizi zilichangia asilimia 30.2 ya pato la Taifa na inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wanategemea sekta hii kwa kuwapatia ajira na mapato.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kutekeleza azma yake ya kuleta Mapinduzi ya kilimo nchini Wizara imeweza kufanikisha mambo yafuatayo:-

Serikali ya Awamu ya Saba kwa kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili itaendelea kulipa kipaumbele suala la kuwapatia wakulima ruzuku kwenye nyenzo na pembejeo za kisasa (mbegu bora, mbolea, dawa na huduma za matrekta) ili kuinua uzalishaji hasa kwa mazao ya chakula ikiwemo mpunga na mboga mboga. Aidha, katika kipindi cha misimu ya kilimo 2010 hadi 2013 kumekuwa na ongezeko maradufu la ununuzi na matumizi ya pembejeo hizo kama ifuatavyo:-

Kwa mbegu bora, Serikali imeongeza pembejeo kutoka tani 55 mwaka 2010 na idadi hiyo kuongezeka mwaka hadi mwaka na kufikia tani 620 mwaka 2013, mbolea – *TSP* na Urea kutoka tani 130 mwaka 2010 hadi kufikia tani 1,500 mwaka 2013 na dawa ya magugu kutoka lita 12,000 mwaka 2010 hadi kufikia lita 30,000 mwaka huu.

Kwa upande wa matrekta Wizara ya Kilimo na Maliasili inatarajia kuingiza nchini matreka 20 kutoka Suma JKT ya Tanzania Bara hivi karibuni. Mhe. Spika, katika Mkutano huu jumla ya maswali 57 ya msingi na maswali 123 ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wajumbe na kupatiwa majibu na ufafanuzi wa kina na Waheshimiwa Mawaziri. Nawapongeza kwa dhati Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kuuliza maswali hayo ambayo yalikuwa na lengo la kuwaelimisha wananchi.Aidha, Waheshimiwa Wajumbe walijadili na kupitisha jumla ya Miswada mitatu ambayo ni:-

a) Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Baraza la Vijana la Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo,

b) Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Amri ya Barabara, Sura 134 na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo,

c) Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Kukinga na Kusimamia Masuala ya UKIMWI Zanzibar, Kulinda na Kuendeleza Haki za Watu Wanaoishi au Walioathirika na Virusi vya UKIMWI na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Spika, Mswada wa Kwanza uliowasilishwa kwenye Baraza lako Tukufu na kujadiliwa ni Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Baraza la Vijana la Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Kuwasilishwa kwa mswada huu kunatokana na kilio cha siku nyingi cha vijana wetu wa Zanzibar kutaka kuwa na chombo chao kilichoanzishwa kisheria cha kuwaunganisha na kufuatilia masuala mbali mbali yanayowahusu na ya maendeleo kwa nchi yetu.

Mhe. Spika, madhumuni makubwa ya Mswada huu ni kuwakuza vijana wetu ili wawe wazalendo kwa Taifa lao kwa kuwajenga ili wajitambue, wajiheshimu wao na waheshimu wengine na pia kuitambua kwa kina jamii yao kisiasa na kiuchumi na pia kuuthamini utamaduni wa nchi yao. Aidha, Mswada huu una lengo la kuwaweka pamoja vijana wetu na kuweza kubadilishana mawazo ambayo yatawasaidia wao pamoja na kulisaidia Taifa letu ili liendelee kusonga mbele. Taifa lenye nguvu kazi imara ambayo ni vijana linapata maendeleo kwa kasi sana. Hivyo, nasi hatuna budi kuwakuza vijana wetu kwenye mtazamo wa kizalendo na kimaendeleo ili kuisaidia nchi yetu.

Mhe. Spika, Mswada mwengine uliowasilishwa, kujadiliwa na kupitishwa na Wajumbe ni Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Amri ya Barabara, Sura 134 na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Mswada huu una lengo la kurekebisha Sheria ya Barabara Sura 134 ambapo vifungu vingi vilivyomo kwenye sheria hii haviwezi kufanya kazi kwa wakati tulionao kutokana na kuwa Sheria hii ni ya muda mrefu na baadhi ya vifungu haviendi sambamba na mabadiliko yaliopo ya ufanyaji kazi.

Mhe. Spika, Mswada wa mwisho uliowasilishwa ni Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Kukinga na Kusimamia Masuala ya UKIMWI Zanzibar, Kulinda na Kuendeleza Haki za Watu Wanaoishi au Walioathirika na Virusi vya UKIMWI na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Mswada huu una madhumuni ya kuweka mfumo wa kisheria wa kuzuia na kusimamia masuala yote ya virusi vya UKIMWI na UKIMWI hapa Zanzibar kwa lengo la kuimarisha haki za binaadamu kwa wale wote wanaoishi au walioathirika na virusi vya UKIMWI.

Aidha, kuwepo kwa Mswada huu kutasaidia sana kuweka uratibu mzuri wa masuala yanayohusiana na UKIMWI na Virusi vya UKIMWI kwa Taasisi na Jumuiya zote zinazojishughulisha na masuala haya. Pia, Mhe. Spika, Mswada huu umetoa wajibu wa kila mmoja wetu kuweza kujua hali yake ya Virusi vya UKIMWI kwa kupima afya yake na vile vile, kuweza kujilinda yeye mwenyewe na kuwalinda wengine kutokana na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI. Mswada unasisitiza jamii kujiepusha na mila na itikadi potofu pamoja na mazoea ambayo kwa kiasi kikubwa yanasababisha kuenea kwa Virusi vya UKIMWI.

Ni busara sisi Waheshimiwa Wawakilishi pamoja na wananchi wote tukazingatia sana elimu tunayopata inayohusiana na masuala yote ya UKIMWI ikiwemo masuala ya kinga, maambukizi, huduma na mengineyo. Sote tunaelewa kwamba UKIMWI ni ugonjwa hatari na matibabu yake hadi sasa hayajapatikana. Hivyo, ni bora zaidi kujikinga. Tusidanganywe na watu wanaojidai madaktari wa dawa asilia na wanaweza kulitibu gonjwa hili. Si kweli bado dawa ya aina yoyote haijapatikana pamoja na utafiti wote unaofanyika kuipata dawa ya kuponyesha ugonjwa huu.

Mhe. Spika, Baraza lako Tukufu pia lilipata nafasi ya kujadili kwa kina Ripoti ya Kamati Teule ya Kushughulikia Migogoro ya Ardhi ambayo Mwenyekiti wake alikuwa ni Mheshimiwa Ali Mzee Ali. Nachukua nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati hii pamoja na Wajumbe wake wote kwa kuifanya kazi hii na kuikamilisha na kuwasilisha ripoti yake. Nilihakikishie Baraza lako Tukufu kuwa Serikali imeipokea ripoti hii na itaifanyia kazi ipasavyo.

Hata hivyo, ripoti hii imekuja kinyume na matarajio ya wengi, wakiwemo baadhi ya Wajumbe wenyewe. Maeneo mengi yenye migogoro na malalamiko yameachwa bila ya kuchunguzwa. Muda ambao Kamati hii iliyochukua ilitegemewa ingekuja na ripoti nzuri zaidi. Serikali itaendelea kushughulikia ile migogoro ambayo haikuzingatiwa na Kamati hii na kuchukuliwa hatua muafaka.

Mhe. Spika, Serikali imeyapokea mapendekezo yote yaliomo ndani ya Ripoti ya Kamati na hasa lile linalohusu wananchi kuelimishwa juu ya dhana nzima ya ardhi kuwa mali ya Serikali. Tunakubaliana na pendekezo hili kuwa ipo haja ya kufanya hivyo na Serikali itaendelea kuwaelimisha wananchi ili waielewe vema dhana hiyo. Nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi washirikiane na Serikali katika kutoa elimu hiyo kwa wananchi wao Majimboni.

Mhe. Spika, pamoja na kulipokea pendekezo hili, Serikali pia imeyapokea mapendekezo mengine yote na itayafanyia kazi kadri itakavyoona inafaa.

Mhe. Spika, Pia, Baraza lako tukufu lilipokea hoja mbili za Wajumbe wa Baraza hili zilizowasilishwa na Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura na Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mwakilishi Viti Maalum. Hoja hizo ni:-

a) Hoja ya Mjumbe ya Kuomba ridhaa ya Baraza kwa ajili ya Kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Utawala wa Baraza, na

b) Hoja ya Mjumbe ya kuliomba Baraza Kutoa Azimio dhidi ya vitendo vya udhalilishaji wa watoto, Zanzibar.

Mhe. Spika, hoja zote hizo zilipokelewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu.

Mhe. Spika, hoja inayohusu Azimio dhidi ya vitendo vya udhalilishaji wa watoto ilipata michango mingi kutoka kwa Wajumbe wa Baraza lako, na kwa kweli ilistahili kupata michango hiyo kwani suala la udhalilishaji wa watoto ni jambo baya na la kukera sana na linatia aibu nchi yetu.

Na ndiyo maana Wajumbe waliichangia hoja hii kwa uchungu mkubwa. Naviomba vyombo vya sheria vitende haki kwa kuwachukulia hatua kali wale wote watakaothibitika kufanya vitendo hivyo, imetolewa hapa na Waheshimiwa Wajumbe, mifano mingi mingine ni ya aibu na ya kutisha. Hatuwezi kuvumilia kuwa na watu wa aina hiyo ndani ya jamii yetu. Napenda nimpongeze sana Mjumbe aliyetuletea hoja hiyo hapa Barazani. *(Makofi).*

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena nichukue nafasi hii kukupongeza tena wewe binafsi, wasaidizi wako pamoja na watendaji wote wa Baraza kwa kuhakikisha kwamba shughuli za Baraza zilizopangwa zote zinatekelezwa chini ya maelekezo na busara zako Mhe. Spika. *(Makofi).*

Mhe. Spika, vile vile, niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili kwa jinsi wanavyojadili hoja mbali mbali zinazowasilishwa kwenye Baraza kwa umakini wa hali ya juu. Michango na hoja wanazoziibua zinatusaidia kuweza kufanya kazi kwa upeo mkubwa.

Mhe. Spika, kabla kumaliza hotuba yangu naomba nitoe pole nyingi sana kwa Mwakilishi mwenzetu Naibu Waziri wa Afya kwa kufiwa na mama yake mzazi, ninamuomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahala pema peponi.

Mhe. Spika, Mwisho kabisa navishukuru vyombo mbali mbali vya habari, radio, *television* na magazeti kwa kuwa nasi kwa kipindi chote cha Baraza hili. Pia, nawashukuru, wakalimani wa alama kwa kazi yao nzuri waliyoifanya ya kuwawezesha wananchi wenye ulemavu wa kusikia kujua nini kilichokuwa kinaendelea ndani ya Baraza hili.

Pia, Mhe. Spika, niwashukuru Wajumbe wote kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa utulivu na umakini mkubwa kwa muda wote wa Baraza hili. Ninawatakia safari ya salama kurudi Majimboni mwao kuwatumikia wananchi wao.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kutoa hoja ya kuliakhirisha Baraza lako Tukufu hadi tarehe 22 Januari, 2014 saa 3.00 barabara za asubuhi panapo majaaliwa.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kwa hotuba hiyo ambayo imejumuisha mambo yote ambayo yalikuja kufanyiwa kazi katika ukumbi huu kwenye mkutano huu wa 14.

Waheshimiwa wajumbe kabla sijawahoji juu ya suala la kuakhirisha mkutano huu, naomba niseme mambo mawili. Moja kumshukuru sana Mhe. Makamu wa pili wa Rais, kutoa hutuba ya kutufungia mkutano wetu huu. Lakini pili, kuungana nae Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kuwashukuru watendaji wote wakiongozwa na Katibu wa Baraza la Wawakilishi kwa kazi nzuri ambayo wameitayarisha kumaliza shughuli zetu zote hizi.

Lakini niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote pamoja na Mawaziri kwa kazi ambayo tumeshirikiana kuanzia tulipoanza mkutano huu wa 14 hadi leo hii tunapomalizia mkutano wetu huu, Waandishi wa habari wamekuwa nasi kwa muda wote pamoja na ndugu zetu wale ambao wanatoa tafsiri kwa wenzetu ambao hawasikii.

Ninawashukuru watendaji ambao mara kwa mara walikuwa wanahudhuria kwenye vikao vyetu hivi ili kuona shughuli zinafanyika hapa na maelekezo ambayo yanatolewa na Baraza hili.

Waheshimiwa Wajumbe jambo la pili baada ya shukurani hizo kama kwa siku tatu hivi mlikukwa hamnioni katika shughuli za Baraza na niliona niende Dodoma baada ya kushauriana na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, baada ya kuona kwamba kumekuwa na ukimwa mkubwa, juu ya suala zima muhimu ya masuala ya Bunge Maalum la Katiba. Ili kujua kuna matayarisho gani nini

kinatendeka, yepi yanayofanyika na mengine mambo gani ambayo bado hayajafanywa. *(Makofi).*

Safari hiyo ilikuwa na mafanikio kiasi baada ya kuonana na Mhe. Spika, na kutaka kujua nini ambacho kinaendelea kwa mambo mbali mbali yanayohusu matayarisho ya Bunge hilo la Katiba. Na kimsingi baada ya kuzungumza na mwenzangu Mhe. Spika, Anna Makinda, tumekubaliana kuanzia siku ya Jumatatu Katibu wa Baraza la Wawakilishi na timu yake wataondoka kwenda Dar es Salaam ili kuanza rasmi mipango mbali mbali ya matayarisho ya Bunge hilo.

Hii ni pamoja na masuala na mambo yanayohusu Kanuni, mambo yanayohusu bajeti ya Bunge hilo, na hatimae mambo yanayohusu mapokezi ya wajumbe wa Bunge hilo Maalum la Katiba pale Dodoma

Tunayo taarifa kwamba Bunge hili litaketi pale Dodoma ukumbi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yataranyika ili kuona kwamba shughuli hiyo itafanyika na katika muda ambao unakusudiwa yafanyike. Sasa tumekubaliana kwamba kazi ya utendaji pale ambapo watafikia pahala basi tuitake mara kwa mara ili kuona hatua kwa hatua juu ya mpango kazi ambao watakaa kuanzia siku ya Jumatatu mpaka kuona kwamba shughuli za matayarisho yote ya Bunge la Katiba yatakuwa yamekamilika na mapokezi ya wajumbe yawe yamekamilika, pamoja na sehemu za kukaa wajumbe hao mbali mbali.

Hayo ndio katika mambo ambayo tulikwenda nayo na kumtaka mwenzangu basi mambo haya yachukuliwe hatua haraka iwezekanavyo ili yakidhi haja kwa mujibu wa ratiba ambayo itakuwa imepangwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba katika kutayarisha Bunge hilo Maalum la Katiba.

Niliona Waheshimiwa Wajumbe niwape taarifa hiyo kwa sababu kulikuwa na ukimya mrefu na katika mambo tuliyokubaliana pia tukaona kuna haja kubwa ya kuwepo mafunzo juu ya hasa hasa kanuni ambazo zitakuja kupitishwa hapo baadae. Kwa hivyo, ni mafunzo kwetu sisi, kwa upande wa Bunge na wale wengine ambao watakuja kuteuliwa baada na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hayo ni mambo muhimu ili kuona jambo hilo muhimu kwa nchi yanafanyika na kwa mujibu wa wakati ulivyopangwa.

Basi Waheshimiwa Wajumbe niliona nitoe taarifa hiyo muhimu ili tuone kwa kiasi gani mabadiliko katika nchi yetu hasa kuhusiana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yatakuwa yamefanyika, mambo ambayo sisi pamoja na wabunge wengine ambao watateuliwa baadae na wale Wabunge wa

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini hatimae na kwa wananchi wote itakuwa ni kazi ambayo tunaifanya sisi.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Saa12.27 jioni Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 22 Januari, 2014 saa 3.00 asubuhi)